CHUO CHA BIBLIA

UTANGULIZI WA INJILI
NA
UCHAMBUZI WA KITABU CHA MATHAYO

KITABU CHA KUMI

SURA YA KWANZA
‘Vitabu Bora Zaidi Katika Biblia’

Vitabu vya kwanza vinne katika Agano Jipya hujulikana kama ‘historia ya maisha ya Yesu’ kwa sababu ndani yake, tunapata habari za historia ya maisha muhimu sana kuwahi kushuhudiwa. Hata hivyo, vitabu hivi vinne sio kama vitabu vya kawaida vya historia ya mtu jinsi huwa tunafikiria. Hii ni kwa sababu mbili kati ya vitabu hivyo havitaji habari kuhusu kuzaliwa kwake wala miaka thelathini ya kwanza ya maisha yake.

Kitabu cha Marko kinasema, ‘Yesu alikuja,’ na hapo baadaye, tunakumbana na Yesu akiwa na umri wa miaka thelathini na kumfuata hadi mwisho wa maisha Yake baada ya miaka mitatu. Jambo hili pia tunaligundua wakati tunaposoma Injili ya Yohana. Mathayo anataja kuzaliwa kwake kwa ufupi huku akionekana kutogusia miaka thelathini ya kwanza ya maisha Yake. Luka ndiye mwandishi wa pekee wa Injili ambaye anatoa habari zaidi kwa kuvunja kimya juu ya tukio moja dogo ambalo lilifanyika miaka thelathini ya kwanza katika maisha ya Yesu. Kusudi kuu la hawa waandishi ni kutueleza kwamba Yesu alikuja - na ni kwa sababu gani alikuja ulimwenguni.

Injili Zinazolingana

Unaposoma vitabu hivi vya Injili, jambo la kwanza ambalo unastahili kutambua ni kwamba, yaliyomo katika vitabu vya Mathayo, Marko na Luka yanafanana au yalingana ilhali asilimia tisini ya yale yaliyomo katika Injili ya Yohana yapatikana tu katika Injili hiyo. Kwa kuwa mengi ya yale yaliyomo ndani mwake yafanana, vitabu hivi vitatu vya kwanza vinajulikana kama ‘Injili zinazolingana.’

Marko anataja ukweli kuhusu Yesu Kristo kwa uwazi kabisa na maelezo sahihi . Hili kupata ufafanusi zaidi katika uandishi habari ulio na uwazi na sahihi, wanafunzi katika vyuo vya Uandishi habari huhitajika kusoma kitabu cha Marko baada ya kusoma vitabu vya Mathayo na Luka. Kuambatana na uwazi wake pamoja na uchuguzi wa habari za kinyume cha Injili hizi, ni maoni ya wasomi wengi kwamba Marko ndiye aliandika kwanza naye alimtumia Petro kama mpashaji habari wake kwa kuwa ndiye aliyehusika katika matukio yote. Kulingana na maoni ya wasomi hao, Mathayo na Luka walitumia Injili ya Marko kama msingi wa Maandiko yao. Ni dhahiri kwamba waandishi hawa wa Injili ya kwanza na ya tatu waliamini kwamba kulikuwepo na mtazamo wa maisha ya Yesu ambao Marko hakuandika katika nakala yake. Waliongozwa na Roho Mtakatifu kuandika Injili zao kwa kuwa walitaka kushiriki pamoja nasi.

Kwa kuwa asilimia tisini ya yale yaliyomo katika Injili ya Yohana hayapatikani katika Injili za Mathayo, Marko na Luka, ni dhahiri kwamba mtume Yohana alitaka kuelezea juu ya maisha na huduma yake Yesu Kristo ambayo hayapatikani katika Injili nyingine tatu. Na kwa sababu hiyo, Injili ya Yohana ni ya kipekee kwa sababu nyingine nyingi ambazo tunazitambua katika uchambuzi wetu.

Maisha ya Yesu ni msingi wa historia ya mwanadamu. Sehemu kuu ya ulimwengu hugawanya historia kabla ya kuzaliwa kwa Yesu na baada pamoja na kuishi kwake. Chukua jarida au gazeti lo lote na hakika litakuwa na tarehe ya siku iliyochapishwa. Tarehe hilo ni utambulisho wa miaka ambayo imekuwepo tangu maisha ya Yesu Kristo. Baada yetu kuchuguza na kuelezea kwa muhtasari hadithi hii ya historia ya Yesu kwa pamoja, tutakuwa tumeupokea ufahamu zaidi katika maisha ya Mtu huyu, ambaye alipata kuishi tu kwa miaka thelathini na tatu na kufanya kishido kikuu katika historia ya ulimwengu huu.

Ufunguo Kwa Maandiko

Baada ya kusulubiwa na kufufuka katika wafu, Yesu alifanya mazungumzo na mitume wake. Tunasoma kwamba aliwaambia jambo fulani kuhusu Maandiko ambalo lilifungua ufahamu wao wa Neno la Mungu. Ingawa walikuwa naye kwa muda wa miaka mitatu, mitume hawa hawakufahamu Maandiko.

Ni jambo gani ambalo Yesu aliwaambia kuhusu Maandiko ambalo liliufungua mawazo yao kwa Neno la Mungu? Tunasoma kwamba: '*Akaanza kutoka Musa na manabii wote akawaeleza katika Maandiko yote mambo yaliyomuhusu yeye mwenyewe* (Luka 24:25-27, 44, 45).' Wakati waliposikia kwamba Maandiko yalikuwa kumhusu Kristo, kwa mara ya kwanza katika maisha yao, wale mitume waliyafahamu. (Ni wazi kwamba alikuwa akigusia kuhusu Agano la Kale wakati alipowaambia kwamba Maandiko yote yalikuwa kuhusu Yeye).

Yesu pia aliwaambia waandishi na Mafarisayo kuwa: *'Mwayachuguza Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia. Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima* (Yohana 5:39,40).'

Oswald Chambers, mwandishi kutoka Uingereza wa vitabu vya Injili aliamini kwamba mistari hii miwili ndio ufunguo katika Biblia nzima. Kwa hakika, hatutafahamu Biblia hadi tutakapotambua kwamba Agano la Kale na Jipya ni kuhusu Yesu Kristo! Biblia sio historia ya ustaraabu. Pia Biblia haitakikani kuwa kitabu cha sayansi kuhusu maumbile. Bali Biblia ni kitabu kuhusu wokovu na ukombozi. Kusudi la Biblia ni kudhihirisha Yesu Kristo kama mwokozi na mkombozi wetu, na kutupatia hali ya kihistoria ambayo kupitia kwayo, Mwokozi na Mkombozi wetu alikuja ulimwenguni.

Ikiwa viongozi wa dini walihitaji masikio ya kiroho hili kumsikiza Yesu, wao wangepokea ufunguo kutoka kwa Yesu ambao ungefungua ufahamu wao wa Maandiko ya Agano la Kale. Na macho yao yangefunguliwa na kuona muijiza kwamba Masihi alikuwa amesimama mbele zao.

Ukweli huu kwamba Biblia nzima inahusu Yesu Kristo, unaweza kuleta ufahamu wa Agano zote mbili - agano la kale na jipya siku hizi. Injili hizi nne zina umuhimu mkuu katika Biblia, kwa kuwa kitabu hiki kinahusu Yesu Kristo, na hizi Injili nne ni historia ya maisha ya Yesu.

Maana Ya Injili

Yale yote tunayoamini yanafaa kuanza kwa ufunuo mkuu wa ukweli ambao Mungu ameupatia ulimwengu huu ambao ni maisha na mafunzo ya Yesu Kristo. Moja wapo ya injili hizi itatuambia kwamba, *'Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mungu Mwana wa pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua* (Yohana 1:18).' Neno la Kiyunani ambalo limetafsiriwa kutokana na neno 'aliyemfunua' maanake ni 'kutoa ukweli nje.' Kutoa ukweli katika Maandiko, kunamaanisha kutoa katika msitari huo, ukweli wote.

Tunafahamishwa kwamba Yesu Kristo alitoa nje katika uhusiano wa karibu wa kifuani chake Mungu ukweli ambao sote tunaweza kumfahamu. Hii inamaanisha kwamba Yesu Kristo alikuwa ufunuo mkuu zaidi wa ukweli ambao ulitoka kwa Mungu na kuwasilishwa ulimwenguni. Chote alichokuwa nacho, chote alichokuwa akitenda, pamoja na alichokuwa akisema 'kilitoa nje ukweli wote' kuhusu Mungu. Vitabu vya Injili ni muhimu sana katika Biblia kwa sababu vinatufunza kuhusu Yesu, ambaye ndiye aliyemdhihirisha Mungu kikamilifu.

Kuna msitari mwingine katika Injli ya Yohana ambao unatuambia maana ya Injili hizi nne. Yohana anaandika hivi, *'Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa ni Mungu* (1:1).' Baadaye katika sura hiyo, tunasoma kuwa, '*Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli* (14).'

Hili kuelezea vyema msitari huu, ninakualika kutumia mawazo yako. Wazia kuwa una shida na wandudu aina ya chungu. Unapoacha chakula kitamu mezani, kisha urudi nyumbani usiku, meza yako huwa imejaa chungu- hao. Dhania kuwa umeamua kusuluhisha shida hiyo ya wadundu. Umegundua kwamba chungu hao wametoka katika kichunguu nyuma ya nyumba yako. Katika juhudi zako kumaliza chungu-chungu hao, utamwagia mafuta ya taa kichunguu kisha kuwasha moto. Miale ya moto huo itapanda juu ilhali wale vichungu watazidi kuingia

ndani ya kichunguu chao. Moto huo unapozima, wale chungu-chungu watatoka nje tena na punde si punde watakuwa wameingia nyumbani mwako.

Je! Unawezaje kutatua shida hiyo ya chungu-chungu? Shida yako sio kwamba unawachukia wadundu hao. Bali ni kuwa, chungu chungu hao wamejaa kote mezani mwako ambapo unakula vyakula vyako. Kama ingewezekana kuwasiliana na wadundu hao bila shaka ungewasiliana nao hivi, 'Tazameni, sina chuki nanyi. Kile ambacho sikitaki ni kuwaona ninyi juu mezani yangu. Niko tayari kuwapa sehemu kubwa cha chakula hapo nje karibu na kichunguu chenu ikiwa tu mtaacha kuingia ndnai ya nyumba yangu.' Shida yako kuu ni kwamba huwezi kuwasiliana na chungu-chungu. Wewe ni mwanadamu, nao ni wadundu na watu hawawezi kuwasiliana na wadundu.

Hebu zidi kitumia wazo hilo. Kama ungelikuwa unawapenda chungu-chungu sana nawe una uwezo wa kuwafanyia lo lote unalotaka, unaweza kujibadilisha na kuwa chungu-chungu na kuingia katika kichunguu kisha kusema, Naam, ninyi chungu-chungu, yawezekana kwamba mimi nafanana nanyi, lakini mimi si chungu-chungu. Mimi nni yule mtu anayeishi kwenye nyumba lile kubwa pale juu na nina wazo ninalotaka kushiriki nanyi. Niko tayari kujitolea kama dhabihu kwa ajili yenu, ikiwa tutakubaliana. Nitaweka kipande kikubwa cha chakula hapo karibu na kichunguu chenu, ikiwa ninyi mtakubali kutokaribia nyumba yangu!'

Najua kuwa huu ni mfano usiowezekana, ingawa mnaweza kufahamu kile ninachojaribu kuwasiliana nanyi? Neno ndilo gari la wazo. Mungu alikuwa na ukweli aliotaka kuwasilisha kwetu pamoja na agano la wokovu ambalo alitaka kuimarisha nasi. Baba yetu mpendwa wa mbinguni alitupenda kabisa hivi kwamba akajitolea kuwa dhabihu kuu na kutoka mbinguni hili awasilishe kwetu ukweli huo. Lakini, alikuwa Mungu nasi tulikuwa binadamu. Hii ndio sababu Mungu anamwita mwanawe 'Neno' kisha baadaye kutuambia kwamba Neno hilo lilifanyika kuwa mwili na kuishi kati yetu kwa miaka thelathini na tatu.

Ni jambo la kushusha moyo sana kwa mtu kufanyika chungu-chungu hili kuwasiliana na chungu-chungu, na kujitolea kuwa ni dhabihu kwa ajili yao. Hata hivyo, wakati Biblia inapotufunza kwamba Mungu alifanyika mwili hili aweze kuwasiliana nasi na kutuokoa tokana na dhambi zetu, huku ndiko kulikokuwa kushushwa ambako kumewahi kuonekana.

Yesu Yuaja! Naam Yesu Njoo!

Shida kuu inayokambiliwa katika Biblia ni kuhusu mwanadamu aliyejitaliki kutoka kwa Mungu na kuwa talaka hiyo ni lazima ipatanishwe. Ujumbe wa Agano la Kale unajumuisha suluhisho kwa shida kupitia maneno: 'Yesu yuaja!' Ujumbe wa Agano Jipya unaeleza suluhisho kwa shida kupitia maneno mawili: 'Yesu Alikuja.'

Kote katika Agano la Kale, tunasikia manabii na wengine wakisema, 'Ni nafahamu kwamba itatendeka. Namwamini Mungu wakati Neno lake linapotuambia kwamba atamtuma Masihi humu duniani.' Tunasikia watu kama Ayubu wakitabiri, 'Mimi nafahamu kwamba mkombozi wangu aishi, na siku moja atasimama juu ya nchi.' Hata hivyo, tunamsikia Ayubu akilia na kusema, *'Ee, laiti ningeweza kufahamu mahali naweza kumpata* (Ayubu 19:25; 23:3).'

Katika Injili hizi, tunasikia watu kama Andrea, nduguye Simoni Petro, akitangaza kuwa*, 'Tumempata Masihi!* (Yohana 1:41).' Na wakati mwanamke msamaria anasema kwamba Masihi atakuja hivi karibuni, tunamsikia Yesu akimjibu kwa uwazi kabisa, 'Mimi ndiye.' Anasema kwamba kwa hakika Yeye ndiye Masihi aliyeahidiwa na manabii katika Agano la Kale (Yohana 4:25,26).'

Vitabu vya kwanza vinne vya Agano Jipya vinaitwa 'Injili' kwa kuwa neno 'Injili' linamaanisha 'Habari Njema.' Wakati mitume wanapoelezea kwa muhtasari matumizi ya Habari Njema ya Injili hizi, kunaelezewa kwamba Mungu amepatanishwa nasi kwa kuwa Yesu alikuja. Habari hizi zinajumuisha changa moto ya vitabu hivi vya historia ya Yesu Kristo kwa njia hii: *'Mungu atutumia hili kuzungumza nawe: basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba*

Mungu anaishi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu (2 Wakorintho 5:20).'

Tunapokagua Agano Jipya kwa pamoja, ni ombi langu ikiwa umetenganishwa na Mungu, utakuwa na ufahamu wa kupatanishwa Naye kupitia Yesu Kristo. Unapopatanishwa na kurejeshwa katika uhusiano na Mungu kumpitia Kristo, basi unaweza kupatanishwa na watu wengine. Hiki ndicho kina kikuu cha ujumbe wa Agano Jipya.

Utafute huo ujumbe unapoisoma Agano Jipya. Ujumbe huo ni: Amani na Mungu, Amani kwako binafsi, na amani pamoja na watu wengine, kwa kuwa wewe unamwamini Yesu Kristo Masihi aliyekuja katika ulimwengu wetu.

SURA YA PILI
'Ujumbe Wa Huduma Ya Yesu'

Tunaposoma Injili kwa utaratibu, huwa tunavumbua kwamba Yesu alikuwa Mtu mwenye huduma, na kwamba alifahihamu kazi yake. Unaposoma Injili pamoja nami, msikilize Yesu akisema sababu yake kuja. Utamsikia akielezea 'shauku kuu' yake. Jinsi anavyoelezea sababu kuu ya maisha na huduma yake kwa uwazi, hakutakuwa na shaka kuhusu Yeye ni nani na sababu yake kuwa hapa ulimwenguni. Kwa mfano, katika Injili ya Yohana tunamsikia Yesu akitangaza mwito wake pamoja na malengo yake kwa njia hii: *'Imetupasa kuzifanya kazi zake Yeye aliyenipeleka maadamu ni mchana; usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi* (9:4).' Tena, tunasikia Yesu akiwaambia mitume wake*, 'Mimi nina chakula msichokijua ninyi . . . Chakula changu ndicho hiki, niyatende mapenzi yake aliyenipeleka, nikaimalize kazi yake* (4:32, 34).'

Alipomaliza miaka mitatu katika huduma Yake, Yesu alikwenda hadi kwenye bustani la Gethsamane na kuomba hivi: *'Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye* (17:4).' Maneno yake ya mwisho juu ya msalaba yalikuwa kilio kikuu cha ushindi, 'Imekwisha! (19:30).'

Kusudi La Maisha

Yesu aliishi maisha yaliyokuwa mfano ambao ulituonyesha kusudi la maisha ya binadamu. Itikadi inayotambulikana sana mbayo hufundishwa watoto wa wazazi wanao mcha Mungu inasema: 'Kusudi kuu lake mwanadamu ni kumtukuza Mungu, na kumfurahia Yeye milele.' Kusudi la maisha ya binadamu ni kumtukuza Mungu. Lakini, hii inamaanisha nini, na ni jinsi gani tunamtukuza Mungu?

Yesu alijibu swali hilo wakati alipofanya maombi haya, Jitukuze Mwenyewe, Baba, na unitumie mimi stakabadhi - Mimi nitayari kuilipa dhamana yake (Yohana 12:23-28).' Alionyesha ukweli, kwamba kwa kuishi maisha yale aliyoishi, Alilipia thamani ambayo ilimtukuza Mungu, ambapo mwishoni mwa maisha yake, alitangaza: *'Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye. . . Imekwisha!. . . Baba, katika mikono yako naiweka roho yangu* (Yohana17:4; 19:30).'

Katika mwongo wa mwaka wa 1950, kijana mmoja kwa jina *Jim Elliot*, na wamishionari wengine wanne ambao walikuwa naye nchini Ecuador- Marekani Kusini- waliuawa wakati watu wa jamii ya kihindi - Auca - walipowavamia kwa upanga, na kutupa maiti zao mtoni kwenye mbuga. Wakati askari wanajeshi walipotumwa kwenda kuwatafuta, walipata maiti ya Jim Elliot, na kijitabu chake cha shunguli za kila siku. Katika kijitabu hicho, walisoma maneno hayo: 'Wakati utakapofikia mipango na malengo yake Mungu kwako, hivi kwamba upate kufariki, hakikisha kwamba cho chote unachohitaji kutenda ni kufariki.'

Tunapokagua Agano Jipya pamoja, lengo langu litakuwa dhahiri ninapokuuliza maswali ya matumizi ya kibinafsi kama: 'Yasema nini? Inamaanisha nini? Inamaanisha nini

kwako? Je! Inamaanisha nini kwa watu wale ambao wamo katika uhusiano? Je! inamaanisha nini kwa watu ambao unawafundisha, na je! inamaanisha nini kwa Mungu?'

Siku zote za maisha yake, Yesu alikuwa na shauku kuu kuhusu kazi ambazo Babake alitaka Yeye atimize. Siku baada ya nyingine. Alikuwa akisema, 'Ni lazima nimalize kazi Zake aliyenituma kungalipo mchana, kwa kuwa usiku waja wakati sitaweza kuitenda kazi.' Yesu alipomaliza maisha yake, hakuwa amebakisha kazi ye yote. Kile kilichobakia ni kufariki tu.

Unapotekeleza utangulizi huu wa kibinafsi, ningependa kukuuliza baadhi ya maswali:

Ni kipi kilichoanza maishani mwako kama msululu wa yale Yesu alivyomaliza kwa njia ya kuishi maisha yake? Je! Umepata kazi ambayo Mungu alikuamuru na kukuokoa hili uimalize kwa ajili ya utukufu Wake? Je! Umemaliza kazi hiyo siku baada ya nyingine? Wakati muda wako wa kufa unapowadia, je! Utaweza kusema, *'Baba, Mimi nimekutukuza humu ulimwenguni. Nimeimaliza kazi ambayo umenipa kuitenda? Baba, katika mikono yako naiweka roho yangu?'* au, utakuwa na hali yatomaliza kazi ile wakati unapotafakari juu ya lengo ya Mungu kwa wokovu wako katika maisha haya?

Maisha Ya Kristo

Njia bora ya kusoma maisha ya Yesu Kristo katika Injili ni kuuliza swali hili: Ni kazi gani ambazo Baba alimtaka Yeye kumaliza zilizokuwa za umuhimu mkuu kwa Yesu? mwishoni mwa mateso Yake, wakati Yesu alipopaza sauti kuu ya ushindi juu msalabani kwamba 'Imekwisha!' Kwa hakika, Yeye alikuwa ametimiza huduma yake. Lakini ni kitu gani ambacho alimaliza?

Kuna sura themanini na tisa katika Injili hizo nne. Sura nne kati yake zinagusia kuzaliwa kwake na miaka thelathini ya maisha yake. Sura themanini na tano zinagusia miaka mitatu ya mwisho wa maisha yake. Sura ishirini na saba zinagusia juma la mwisho la maisha yake. Sura hamsini na nane zinagusia huduma yake ya mafunzo, uponyaji na kuwaita mitume Wake. Katika Injili ya Yohana, yamkini nusu ya sura zake zinagusia miaka thelathini na tatu ya kwanza katika maisha Yake, ilhali nusu ile nyingine inagusia juma la mwisho katika maisha Yake.

Kwa hawa waandishi wa Injili, miaka mitatu ya mwisho wa maisha Yake ni muhimu sana kuliko kuzaliwa kwake na miaka thelathini ya kwanza. Juma la mwisho katika maisha yake ni muhimu sana mara saba zaidi ya kuzaliwa pamoja na miaka thelathini ya kwanza ya maisha Yake. Sura hamsini na nane ambazo zinagusia mafunzo Yake, uponyaji na kuwaita mitume zinadhihirisha thamani za waandishi walizotilia katika maeneo ya maisha na huduma Yake.

Kwa kuwa ukaguzi wetu wa Agano Jipya sio wa undani zaidi, wala uchambuzi wa masomo yaliyomo katika Injili, bali ni utangulizi na ukaguzi wa juu juu ambao hujaribu kukuonyesha jinsi unavyoweza kukaribia Injili na kukupa picha kubwa, nitajaribu kutilia mkazo uchuguzi wetu ambapo waandishi wa Injili walitilia mkazo, katika maeneo yaliyo katika historia hizi takatifu za maisha ya Yesu.

Huduma Kuu Ya Yesu

Uchuguzi wa vitabu hivi utatuonyesha kwamba vinaitwa 'Injili' kwa sababu vinatoa 'Habari Njema' kwamba Yesu alikuja na wakati alipokuja, alikuwa Mwana Kondoo wa Mungu aliyekuja kuchukua dhambi ya ulimwengu (Yohana 1:29). Ikiwa tunafahamu kwamba tu wenye dhambi, basi tutafahamu sababu ya hawa waandishi kufikiria kwamba hii ni 'Habari Njema.'

Sura nyingi katika vitabu hivi zinatilia mkazo juma la mwisho katika maisha ya Yesu, kwa kuwa ni katika juma hilo moja alipotenda yote yaliyohitajika kutoka kwake kama Mwana Kondoo wa Mungu, hili kutuokoa kutokana na dhambi zetu. Mkazo mkuu katika Injili hizi unatuonyesha kwamba kifo chake juu msalabani huko Yerusalemu kwa ajili ya dhambi zetu na Ufufuo katika wafu ulikuwa mwito mkuu Wake, hivyo basi, ndio thamani au shauku kuu ya kazi Yake.

Theluthi moja ya yote yaliyomo katika Injili ni nakala ya jinsi Yesu alivyotimiza mwito mkuu ambao alikuwa ameagizwa na Babake wakati Mungu alipoupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee kuja na kufa juu ya msalaba kwa ajili ya wokovu wetu (Yohana 3:15-19). Mitume walitilia mkazo umuhimu wa kazi ya wokovu wa Yesu (1 Petro 1:18,19; 2:24; 2 Wakorintho 5:19, 21-6:1, 2).

Huduma Zingine Mbili Za Nia Ya Yesu

Tunaposoma jinsi Yesu alibadilisha Mwongozo mkuu na kuwa malengo ya mwito Wake, kuna maeneo mawili zaidi katika maisha na huduma Yake ambayo yametiliwa mkazo katika Injli. Tunagundua malengo hayo mawili ya kwanza tunapozidi kusoma kuhusu maeneo ya kimiujiza katika maisha na huduma Yake, ambayo ni mkazo wa waandishi wote wanne wa Injili. Yesu alitenda miujiza mingi ambayo ilikuwa ya uponyaji.

Ikiwa tuligundua nakala hizo na hatukuwa na wazo ni kuhusu nini, tunaposoma Injili, tunaweza kufikiria kwamba kichwa mwafaka ni, 'Miujiza ya Yesu,' au, 'Uponyaji wa Yesu.' Kama theluthi moja ya yaliyomo katika Injli hizi nne, inaeleza kuhusu miujiza ya Yesu. Ni jambo la muhimu kwamba kutilia mkazo huku kunazidi chini ya huduma ya mitume hadi kizazi cha kwanza cha Kanisa Lake.

Unaposoma hadithi moja hadi nyingine kuhusu miujiza na uponyaji ambao Yesu alitenda, na kuwaona mitume katika kizazi cha kwanza cha Kanisa wakitenda miujiza na kuwaponya wagonjwa, jiulize mwenyewe, 'Ni umuhimu gani uliopo katika maeneo haya ya huduma ya Kristo aliyefufuka na kuishi siku ya leo? Ikiwa Yesu yule yule aliyeishi hapa miaka elfu mbili iliyopita na wakati huu anaishi ndani yangu na yako, mwanangu, Je! Unafikiri kwamba anaweza kutenda miujiza na kutuponya siku ya leo?

Kulingana na ufahamu huo ulio nao, Je! Yesu anaifanya miujiza, kuwaponya wagonjwa na kufufua wafu siku ya leo jinsi alivyotenda wakati alipokuwa hapa duniani? Je! Ni mapenzi Yake wakati wote kuponya? Je! Yesu alimponya kila mtu? Je! Yesu alihusika na pia anahusika sana katika miili yetu au katika hali ya kiroho ya watu? Je! Unafikiri jambo vipi? Unapojibu swali hilo katika hali ya uponyaji wa kimwili, kumbuka kuweka kutazamia uponyaji huo wa kiroho unaotokea kupitia wokovu kwa wenye kuamini na kufanyika wanafunzi wa Yesu Kristo siku ya leo.

Ujumbe Wa Yesu

Lengo lingine moja katika mwito mkuu wa Yesu linatiliwa mkazo katika Injili hizi nne, pamoja na kifo chake na ufufuo pamoja na miujiza Yake. Ningependa kumalizia utangulizi huu wa ukaguzi wa Injili na maoni kwamba, yamkini theluthi moja ya yaliyomo katika vitabu vinne vya kwanza katika Agano Jipya, yananukuu maneno yaliyonenwa na Yesu.

Yesu anasema kwamba ndiye Njia, na Kweli, na Uzima, na kwamba hatuwezi kumwendea Mungu Baba kwa njia nyingine (Yohana 14:6). Wakati anapotuambia kwamba Yeye ni Njia ya kumwendea Mungu, huwa anagusia kazi Yake juu ya msalaba ambayo ndiyo iliyoleta njia ya pekee ambayo tunaweza kupatanishwa tena kutokana na talaka yetu kwa Mungu, na hatimaye kurejeshwa kwa uhusiano wetu Naye.

Wakati anapotuambia kuwa Yeye ni Uzima, huwa anagusia miujiza Yake, pamoja na kutupa uzima wa milele na kubadilisha maisha ya wote wenye kumwamini waliofanywa wazima kiroho, hisia pamoja na mwili.

Wakati anapokiri kwamba ni Kweli, kwa hakika, anazungumzia kuhusu huduma Yake ya kufundisha na kuhubiri.

Kama Mwana wa Mungu, Yesu Kristo angelitoka huko mbinguni alasiri moja ya Ijumaa kutoka kwa huduma yake katika hali ya mbinguni na kutimiza wokovu wa ulimwengu kwa muda wa siku chache tu. Ni kwa sababu gani aliishi miaka thelathini na tatu hapa ulimwenguni? Ni lazima kwamba alikuwa na huduma nyingine za kutimizwa kwa ajili ya Babake pamoja na yote yaliyotimizwa kupitia kifo chake juu ya msalaba na ufufuo.

Wakati Yesu alipotuambia kwamba Yeye ni Kweli, na wakati Yohana alipomwelezea kama Neno ambalo lilifanyika kuwa mwili (Yohana 1:14), tunaona huduma ya Yesu ambayo kwa hakika haingetimizwa kwa siku moja ikitiliwa mkazo. Mungu tayari alikuwa ametupatia Neno Lake lililoandikwa. Yohana anaeleza yale Yesu aliyotupatia kwa njia hii: *'Kwa kuwa torati (sheria) ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo* (Yohana 1:17).' Mungu tayari alikuwa ametupatia ukweli kupitia Musa na Agano la Kale. Hata hivyo, kupitia Yesu Kristo, Mungu alitupatia Neema ya kuishi kulingana na kweli hiyo. Yesu hakutupa ukweli peke yake, bali mwenyewe alikuwa ndio ukweli huo aliotupa. Hakutuambia tu jinsi ya kuishi bali pia aliishi maisha hayo- Alikuwa Uzima huo. Kile alichokuwa, alichotenda na alichosema kilikuwa Kweli ambayo Mungu alitaka kuwasiliana nasi kupitia Mwanawe. Hii ndiyo sababu Injili ya Yohana inamweleza Yesu kama kuwa Neno linaloishi.

Tayari tumeona kwamba ujumbe mkuu ambao Mungu amewahi kunena ulimwenguni Yesu Kristo. Sehemu ya ujumbe huo aliosema au kufunza linachukua theluthi moja ya yale yaliyomo katika Injili zote nne. Ujumbe huu wa Yesu unatujia kwa mifumo mingi. Kuna mijadala mingi kama mahubiri ya mlimani, mjadala uliokuwa katika chumba cha orofani na mjadala uliokuwa katika mlima wa Oliveti (Mathayo 5, 6, 7; Yohana 13-16; Mathayo 24:25).

Kuna mijadala mingine hasa katika Mathayo na Luka, ambayo kama manabii wadogo, sio ya thamani duni ikilinganishwa na mijadala mikuu kwa ajili ya ufupi wake. Mingi katika mijadala hii ilikuja katika mifumo ya misemo, hadithi za mafumbo na njia ya majadiliano. Mjadala ulikuwa wakati mwingi wenye uhasama kati ya viongozi wa dini. Utapata mijadala mingi ya aina hii katika mazungumzo mengi ya Yesu. Mengi ya mazungumzo yake yalitokana na maswali aliyouliza katika mazingira ambayo aliwahoji watu.

Unaposoma Injili, wakati Yesu anaposema kitu, kiwe ni katika mjadala mkuu, hadithi za mafumbo, maombi, maswali, majibu, mahojiano, au mijadala yenye uhasama, kumbuka kwamba Yeye ndiye Neno la Milele la Mungu lililofanyika mwili, na kuishi miongoni mwetu. Yeye anapozungumza, huwa anamdhihirisha Mungu kwetu. Atatupatia ufunuo kamili wa Mungu ambao ulimwengu umewahi kupokea (Yohana 1:18).

Njia bora ya kukumbana na kweli yote ambayo imefunzwa na Yesu ni katika kukaribia mafunzo yote Yake akiuliza swali hili? Kulingana na mafunzo Yake, bila kujali mfumo ambao alitumia, au kudhihirisha, ni zipi zilizokuwa thamani za Yesu Kristo?'

Unaposoma Injili, tafuta mwito mkuu wa Yesu Kristo ambao unatimizwa kwenye msalaba tunapokutana naye kama Njia ya kumpatanisha mwanadamu na Mungu. Pia tazama miujiza Yake, hasa miujiza ya kufanywa upya na uponyaji, ambayo inamdhihirisha kama Uzima. Pia, tazama huduma ya mafunzo Yake wakati Neno la Mungu lilifanyika mwili na kuishi pamoja nasi, likijawa na neema na kweli. Soma Injili hili kuona Yesu kama Njia, Kweli, na Uzima.

Uchambuzi Wa Injili Ya Mathayo

SURA YA TATU
'Mpango Wa Yesu'

Katika Injili zote nne, Yesu haonekani tu kama mtu mwenye mwito. Pia anadhihirishwa kama mwenye mpangilio mwafaka wa kutimiza mwito huo. Hii ni wazi hasa katika Injili ya Mathayo.

Ikiwa ungefahamu kwamba una miaka mitatu peke yake kuishi, nawe unataka kufikia ulimwengu wote kwa ujumbe, ni jambo lipi ambalo unahitajika kutenda? Yesu alifahamu kwamba alikuwa na miaka mitatu kuishi na alitaka kufikia ulimwengu wote kwa Injili yake.

Akifahamu hivyo, ni lipi alilotenda? Kuuliza na kujibu swali huku tunaposoma Injili ya Mathayo, kutatuwezesha tutambua mpango huo wa Yesu wa kutimizwa kwa malengo yake.

Ikiwa utahudhuria masomo au washa juu ya jinsi ya kuwa kiongozi mwema, na mwenye usanifu mwingi, basi utaambiwa kwamba hili kuwa kiongozi mashuhuri, ni lazima utende haya: Chuguza, Ongoza, Ajibika, Simamia, kisha Sononeka!

Katika Injili ya Mathayo, kila wakati tunaposoma kwamba Yesu alipowaona makutano, aliwahurumia, tunakuwa na picha ya huruma Yake kwa ulimwengu wote pamoja na mpango wa kufikia ulimwengu wote kwa ujumbe wa wokovu. Wakati Yesu alipotazama makutano makubwa kwa huruma, kila mara alikuwa akitenda kitu muhimu katika mpango Wake. Mara ya kwanza ambapo jambo hili linanukuliwa katika Injili ya Mathayo, Yeye alikuwa akiponya kila aina ya maradhi yaliyopatikana kote ufuoni mwa ziwa la Galilaya. Alichuguza mahitaji ya makutano hayo kisha akawaongoza katika, 'faragha ya kwanza ya Kikristo,' pale alitoa ujumbe juu ya mlima (Mathayo 4:23-5:2).

Wakati mwingine ambapo alipotazama makutano kwa huruma, aliwastaajibisha baadhi ya wale walisikiliza mafunzo Yake juu ya mlima na kuwafanya kuwa 'mitume.' Neno hili maanake ni sawa 'wamishionari.' Kuna tofauti kati ya mwanafunzi na mtume. Yesu alikuwa na wanafunzi - wafuasi wengi, lakini alikuwa na mitume kumi na wawili.

Tunaweza kusema kwamba wakati huu alikuwa amefanya uchuguzi, na uongozi pamoja na kuwajibisha baadhi ya wale ambao watautekeleza mpango wake wa kufikia ulimwengu. Tunapofuata utaratibu huu wa mpango Wake kupitia Injili ya Mathayo, tunasoma matukio mawili ambayo karibu yafanane. Kwa mara nyingine, Yeye anatazama makutano kwa huruma, pamoja na wingi wa shuda zao kuwa ni wenye njaa. Mitume wanamjia na kumsihi awaambie wale makutano waende zao hili waweze kununua chakula. Lakini aliwapa changa moto kwa swali hili, 'mnayo mikate mingapi? Anawaambia kwamba sio lazima makutano yale kufukuzwa kwa kuwa wao ni kama wasaidizi na waakilishi *Wao'* wangeshughulikia mahitaji yao. Hadithi hii inayofahamika sana, ambayo ni muijiza ambao umenukuliwa katika Injili zote nne, kwa hakika ni hadithi yenye mafumbo kuhusu maono ya umishionari wa Yesu (14:14-36; 15:32-39).

Ikiwa tunaweza kutambua kwamba makutano yale yalikuwa yakiwakilisha ulimwengu pamoja na mahitaji yake yote, - wakati tunapomwona Akiweka mitume aliosaidiana nao kati ya mahitaji ya makutano yale, kwenye mpango mwafaka wa Yesu wakutumiza mahitaji ya ulimwengu. Kukutana na mahitaji ya ulimwengu hakutoki moja kwa moja kwa Mungu hadi kwa makutano. Mungu humtumia Yesu Kristo hili kutimiza mahitaji ya makutano yale kupitia mikono ya mitume! Huu ndio mpango wake hata siku ya leo. Kristo aliyefufuka huchagua kuwatumia wanafunzi wake hili kupitisha Kweli na Injili kwa wote ambao wanahitaji wokovu.

Ni dhahiri kwamba maelezo ya hadithi hii ni muijiza iliyovuviwa ambao watu, mahali, na vitu vilivyomo ni vina maana zaidi. Mpango mwafaka wa Yesu ambao unadhihirishwa katika muijiza huu unajitokeza kikamilifu hapo mwishoni mwa Injili ya Mathayo wakati Mathayo ananukuu jinsi Yesu alipotoa Agizo Kuu (Mathayo 28:16-20). Wakati Yesu alikuwa karibu kupaa mbinguni, aliwaagiza watu hawa kufikia ulimwengu kote kama wasaidizi wake.

Tunaweza kusema kwamba baada ya kupaa kwake, Yesu alichukua hatua mbili za mwisho za kiongozi mashuhuri - kusimamia wanafunzi Wake kwa miaka elfu mbili kuendelea ya historia ya Kanisa, huku wao wakifikia ulimwengu kwa ajili Yake. Hivyo basi, ni sawa kusema kwamba pia Yeye amesononeshwa kwa juhudi zao. Hii ni kweli zaidi hasa nyakati za dhiki wakati walipoteswa katika miaka mia tatu ya karne za kwanza ya historia yao. Tunaweza kukubaliana kwamba amezidi kusononeka wakati dhiki imeendelea kwa zaidi ya miaka elfu mbili ya historia ya Kanisa na sehemu nyingi kote ulimwenguni wa sasa. Tunaweza kukubaliana kwamba Amesononeka kuhusu nyakati mbovu katika sura ya historia ya Kanisa ambayo imenakiliwa.

Hii inaweza kutusaidia kufahamu Kanisa la siku ya leo. Tunaweza kuona kusudi sahihi la Kanisa wakati tunapomwona Yesu akitekeleza mpango Wake katika Injili ya Mathayo.

Kanisa ni shirika la umishionari! Kanisa limebuniwa na kupewa uwezo na Kristo hili kuwa chombo ambacho neema na kweli ya Yesu Kristo inatangazwa ulimwenguni. Mipango, miradi na shughuli zote za Kanisa zinahitajika kuwa vyombo vya kutekeleza wajibu huo.

Uthibitisho mkuu wa kweli hii upo katika kitabu cha Matendo. Injili ya Mathayo inamalizia na Yesu akitoa mwito kwa Kanisa lake kwenda kote na kuhubiri Injili kwa ulimwengu uliopotea. Na wanapokwenda, wanahitajika kufanya wanafunzi, kuwabatiza na kuwafundisha kila kitu Yesu alichowafunza. Katika kitabu cha Mathayo hayo ndio waliyotenda. Katika siku ya Pentekoste walipokea Uwezo wa Mungu - na ni katika kutekeleza Agizo hii Kanisa likazaliwa.

Kitabu cha Matendo kwa hakika ni nakala ya jinsi walikwenda kote ulimwenguni, na kufanya wanafunzi, kuwabatiza, na kuwafundisha yote Bwana aliyowafundisha. Kitabu cha Matendo pamoja na historia ya Kanisa kinatueleza kwamba mpango mwafaka wa Yesu Kristo unafanya kazi. Sisi ambao tunaunda Kanisa Lake siku ya leo, bado tuna Agizo la kwenda na kufanya wanafunzi, kuwabatiza na kufundisha yale yote ambayo Yesu alitufunza.

SURA YA NNE
'Matukio Muhimu Katika Maisha Ya Kristo'

Hakuna mhusika ye yote katika Biblia ambaye ana umuhimu mkuu aliyepewa nafasi ndogo kuliko Yohana Mbatizaji. Yesu alisema kwamba huyu mtu alikuwa nabii mkuu zaidi kuwahi kuzaliwa na mwanamke (Mathayo 11:11; Luka 7:28).

Maisha ya Yohana Mbatizaji yanaelezwa kwa muhtasari tu katika Injili zote nne. Umuhimu wa maisha yake ni upi? Kwanza, sio kwamba alikuwa tu nabii mkuu zaidi ya wale wengine. Alikuwa pia nabii wa mwisho. Manabii walihubiri Habari Njema kwamba Masihi alikuwa anakuja. Huyu nabii kwa hakika alimnyoshea mkono Mtu aliyekuwa akipita huko njiani Galilaya na kuwaambia wanafunzi wake, *'Yule Pale! Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu*! (Yohana 1:29).' Yohana alikuwa ndiye nabii wa mwisho kati ya wale waliokuwa wa Kimasihi ambaye kwa hakika alimtambulisha Masihi kwa watu wa Mungu.

Ubatizo Wa Yesu

Kuna matukio kadhaa muhimu katika maisha ya Yesu Kristo ambayo yaelezwa hapo mwanzoni mwa sura za kwanza za Injili ya Mathayo, Marko, na Luka. Siku moja Yohana alikuwa akiwabatiza watu alipomwona kijana amepiga foleni. Wakati Yohana alipomwona Yesu, alisema, 'Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu?' Lakini Yesu akamwambia 'La, ni lazima tuitimize haki yote, Yohana. Wewe unibatize Mimi.' Hivyo basi, Yohana akambatiza Yesu. Wakati alipofanya hivyo, Roho alishuka juu Yake kwa mfano wa hua naye Mungu Baba akanena: 'Huyu ndiye Mwanangu Mpendwa, nipendezwaye naye.' Maandiko ya tukio hili yanatajwa kama ushuhuda wa Yohana Mbatizaji (Mathayo 3:17).

Ubatizo Wake ulikuwa sio kama ule wa siku hizi. Ubatizo huo ni mojawapo ya matukio muhimu ya Yesu Kristo. Hii ilikuwa ndio kuzinduliwa kwa huduma Yake ya miaka mitatu kwa watu. Wakati mtu anapochaguliwa kuwa kiongozi wa taifa fulani, sherehe za kuzinduliwa hufanyika. Katika kuzinduliwa kwake, huyu Rais mpya hutoa hotuba ya kuzinduliwa huko. Yesu aliianza huduma yake kwa uzinduzi. Hata hivyo, katika tukio hili, kiongozi alikuwa Mungu Mwenye-Enzi, nayo hotuba ya uzinduzi ilikuwa fupi sana. Ilikuwa hivi: *'Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa* naye (3:17).'

Majaribu Ya Yesu

Katika sura ya nne ya kitabu cha Mathayo, tunasoma kwamba ubatizo wa Yesu ulifuatiwa na tukio lingine muhimu. Roho alimwongoza hadi nyikani ambapo alikumbana na Shetani, baada ya kufunga kwa siku arobaini, na kujaribiwa mara tatu. Kwanza, yule mjaribu

wake alimjia na kusema, '*Ikiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate.'* Naye akamjibu akasema, Imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.' Neno la kwanza la Yesu lililonakiliwa katika Injili lilikuwa ni, '*Imeandikwa' (*Mathayo 4:4)**.'**

Jaribio la pili lilitokea wakati Ibilisi alipomjaribu Yesu kuruka kutoka kwenye kinara cha Hekalu la Sulemani. Neno linasema, '*Ikiwa ndiwe Mwana wa Mungu, jitupe chini; kwa maana imeandikwa, 'Atakuagizia Malaika zake; Na mikononi mwao watakuchukua; Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe* (6)**.'** Hapa tunaona Shetani akinukulu Maandiko. Kwa hakika anaifahamu Biblia vyema naye hupenda kuwajaribu waaminifu kwa kuleta Maandiko mawazoni mwao hili kuwahukumu, au kuwatia hofu.

Yesu hivi karibuni atatangaza kwamba Yeye ni Mungu katika mwili wa mwanadamu. Je! Ingekuwa vipi kwa mtu ye yote kuamini matangazo hayo? Shetani anamshauri Yesu kutumia uwezo Wake usio wa kawaida hili kuthibitisha tangazo hilo. Lakini Yesu amjibu Shetani, '*Imeandikwa, 'Usimweke Bwana Mungu wako katika majaribu* (7).'

Jaribio la tatu la Yesu ni wakati Shetani alipomwonyesha falme zote za ulimwengu pamoja na fahari zake. '*Haya yote nitakupa ukianguka kunisujudia.'* Naye Yesu akamwambia, *'Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake* (8-10)**.'**

Umuhimu mkuu wa jaribio hilo kwa Yesu huko nyikani ni upi? Kwanza kabisa, naamini kwamba kama kungelikuwa na njia ye yote ya kuepuka Shetani hili kukumbana na Yesu, basi Yeye angekwapa. Tunahitaji kufahamu kwamba Roho Mtakatifu alikuwa akimwongoza Yesu Kristo hili kukumbana na Shetani hapo mwanzoni wa huduma Yake. Kwa lugha ya mafumbo, huyu ndiye 'ndugu mkubwa – Yesu' ambaye anamlipizia kisasi 'ndugu mdogo – Adamu', ambaye alikuwa amefedheheshwa na Shetani katika bustani la Edeni. Jaribio la kwanza kwa hakika ni lile-lile ambalo Adamu na Hawa walikumbana nalo huko kwenye bustani la Edeni.

Jinsi tulivyotambua, Yesu alikumbana na kurudiwa kwa jaribu kutoka Bustani la Edeni kwa kulinukulu andiko: '*Imeandikwa, 'mwanadamu hataishi kwa mkate peke yake, ila kwa kila Neno litokalo kwake Mungu* (Mathayo 4:4)**.'** Kwenye bustani, Shetani aliuliza swali hili, 'Kwa hakika, Mungu alisema hivi? Naye Adamu na Hawa wakamjibu, 'Naam, hivyo ndivyo Mungu alivyo nena.' Na kwa maelezo mengine, huyu Ibilisi alimjibu, 'Naam, yale ambayo Mungu aliyanena siyo ya kweli.' Baada ya kusema kuwa ikiwa Mungu alikuwa amenena hata kidogo, Neno ambalo alilinena lilitiliwa shaka na kupingwa, pamoja na kuwa hakuna aliyelitii.

Je! Unaweza kutambua msemo huu? Yule mwovu hajaacha kamwe kuuliza maswali nyakati zote za historia ya watu wa Mungu. Majaribu haya mawili pia ni maelezo, ya jinsi tunavyojaribiwa kutenda dhambi siku ya leo. Haya pia ni maelezo kuhusu dhambi. Dhambi ni kuhusu kile tunachotenda, au tusichokitenda pamoja na kile tunachofahamu kuhusu yale Mungu aliyonena.

Ukweli muhimu ambao Yesu aalitumia hili kukabiliana na jaribio la kwanza ni kuwa, ikiwa unataka kuishi, Neno la Mungu litakuonyesha jinsi ya kuishi. Vile tunavyozidi kufahamu Biblia, ndivyo tutakavyofahamu maisha. Na jiinsi tunavyozidi kufamu maisha, ndivyo tutakavyozidi kufahamu na kupokea Biblia. Biblia na maisha hutupiana mwangaza moja kwa nyingine. Kusudi la Biblia ni kwamba tupate kufahamu jinsi ya kuishi.

Katika bustani la Edeni, hali halisi ya majaribu ilikuwa kuweka mahitaji ya mwili wako kwanza na katika nafasi ya pili yale Mungu aliyotaka utende. Kwa maelezo mengine, kutafsiri Neno la Mungu kulingana na mahitaji yako. Mungu aliwataka watafsiri mahitaji yao ya kimwili kwa mwanga wa Neno Lake. Na kwa namna fulani, jaribio lile lilikuwa, 'mahitaji yako kwanza, kisha Neno la Mungu kufuatia.'

Wakati Yesu alipojaribiwa kugeuza mawe kuwa mikate, jaribu hilo lilikuwa, 'wewe umekuwa ukifunga kula na kunywa kwa siku arobaini. Tumia uwezo Wako kuweka mahitaji ya

kimwili kwanza, kisha Neno na Mapenzi ya Mungu kuwa pili. Nalo jibu lilikuwa, 'Neno Kwanza, Mahitaji Baadaye.'

Ujumbe wa Biblia wakati mwingi unaweza kufupishwa kwa maneno mawili. Maneno hayo ni: 'Mungu kwanza!' Majibu ya Yesu kwa majaribu yote matatu yanaweza kufupishwa kwa maneno hayo mawili. Kumbuka kwamba majaribu sio dhambi. Jinsi tunavyo kumbana na majaribu ni katika ushindi au katika dhambi. Jinsi tunavyokumbana na majaribu siku za leo pia yahitajika kuwa katika kutimiza maneno hayo mawili – 'Mungu kwanza.'

Katika jaribio la pili, Shetani alinukulu Maandiko na kumshauri Yesu kuthibitisha ikiwa Yeye ndiye Mwana wa Mungu kwa kujitupa chini kutoka juu ya kinara cha Hekaluni la Sulemani. Wazo lilikuwa kwamba, ikiwa Yeye angeokolewa asijikwae, basi kwa hakika angekuwa amethibitisha kuwa Yeye ndiye Mwana wa Mungu.

Kwa mara nyingine, Yesu alikukabiliana naye kwa Maandiko, akimwonyesha Shetani kwamba Mungu alikuwa ametuamuru tusimjaribu. Kuna tofauti ndogo katika kumjaribu Mungu jinsi Gideoni alivyofanya na kumweka Mungu majaribuni (Waamuzi 6:37,38). Tunapojiandikisha katika 'Chuo Kikuu cha Imani' - kule kuikubali changa moto ya kufanyika mfuasi wa Kristo, huwa hatuna haki ya kumjaribu Mungu. Yeye ana haki tutajaribu wakati wo wote jinsi apendavyo, lakini sisi hatuna haki kumjaribu.

Mara ya tatu Shetani alipomjaribu Yesu, alimwahidi falme zote za ulimwengu ikiwa angeanguka na kumsujudia. Kwa mara nyingine, Bwana anatumia Maandiko yanayolingana na yale aliyotoa katika jaribio la kwanza. *'Imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake.'* Hali halisi imo katika maneno hayo mawili: '*Mungu kwanza!'* Mara hii maneno hayo mawili yamebadilishwa na maneno mawili: '*Yeye pekee!'* (Mathayo 4:10).'

Matumizi ya kibinafsi ya majaribu haya matatu ya Yesu kwetu ni dhahiri kabisa. Matumizi ya kwanza ni: 'Mungu kwanza!' Neno la Mungu kwanza, kisha mahitaji yetu baadaye. Mwabudu Mungu peke Yake. Sote tuna nyakati ambazo hujaribiwa kuidunisha imani kwa kuweka Mungu majaribuni, tukisahau Ndiye atayehitajika kutujaribu.

Baada ya Yesu kulipinga jaribio la tatu la Ibilisi, tunasoma kwamba Shetani aliondoka 'kwake kwa kitambo' au kwa muda mfupi. Maneno haya yamaanisha kwamba kulikuwepo na uvamizi wenye nguvu na ukatili mwingi ulioendelea kinyume cha Mwokozi wakati alipokuwa katika kipindi cha mwisho cha miaka mitatu ya maisha yake. Hii ilikuwa ni kweli, hasa wakati alipokuwa katika juma la mwisho, alipokufa na kufufuka tena kwa ajili ya Wokovu wetu.

Wengi hushangaa ikiwa Yesu angeanguka katika jaribio moja kutoka kwa Shetani. Huku Yesu akijaribiwa huko nyikani, je! Mungu Baba alikuwa juu orofani mwake akitizama, akishikilia pumzi, na kuuliza, 'Nashangaa ikiwa atayashinda majaribu yale?' Je! Unafikiri kwamba mambo yalikuwa hivyo? Ninaweza kukuhakikishia kwamba, Mungu alifahamu Mwanawe hangekuwa kama Adamu na kujisalimisha kwa majaribu hayo. Alipojaribiwa huko nyikani, hakuna vile Yesu angetumbukia katika majaribu yale.

Hivyo basi, Mbona akajaribiwa? Ilikuwa jambo la muhimu kwa Mungu kutuonyesha hapo mwanzoni wa maisha na huduma ya Mwokozi wetu, kwamba hangeweza kuanguka. Msitari mmoja wa mwisho katika Biblia unasema hivi kuhusu Yesu Kristo: *'Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu. . .* (Yuda 24).' Ikiwa yule Kristo aliyejaribiwa ambaye hangeshindwa huishi ndani yetu, Je! Anaweza kutulinda kutokana na kushindwa huko? Kwa hakika, Yeye anaweza! Ikiwa tunaweza kumtumainia na kutembea pamoja Naye, Yeye anaweza kutulinda kutokana na kuanguka huko.

Kwa njia aliyokumbana na majaribu Yake, alituonyesha jinsi tunavyoweza kukabiliana na majaribu ya yule muovu. Shetani kwa ukatili mwingi anajaribu kusema kwa kila mmoja wetu kuwa, 'Weka mambo ya mwili kwanza na ya kiroho pili. Weka cho chote kiwe mbele katika maisha yako isipokuwa Mungu.'

Adui mkuu wa kile kilicho bora zaidi ni bora. Hivi ndivyo Shetani hutuambia juu ya yale yaliyo bora kwa Mungu. Hutujaribu kutenda yaliyo bora hili tukapungukiwe na kilicho bora zaidi kutoka kwa Mungu. Kwa kuwa Mungu anatupenda, naye anafahamu kwamba wakati tunapomweka kwanza, Anaweza kutupatia kilicho bora zaidi. Huwa anataka tumuweke kwanza na kushinda majaribu ya Shetani.

SURA YA TANO
'Mahubiri Makuu Ya Yesu'

Yesu alifanya mahubiri makuu mengi. Kwa njia fulani, mjadala Wake mkuu ulikuwa ni Ujumbe wake juu ya mlima. Ujumbe wake juu ya mlima ni muhtasari wa mafundisho ya madili na mafundisho ya uhusiano waYesu. Tunapotilia mkazo hali ambayo mafunzo haya yalitolewa, huwa tunatambua kwamba huu haukuwa ujumbe wa kawaida kama ilivyo siku za leo.

Mazingira Ya Ujumbe

Ni muhimu kutilia maanani mazingira yake kabla ya kutazama hali iliyokuwa katika mjadala huu mkuu wa Yesu. Sheria moja ya usomaji wa Biblia ni kwamba tunahitaji wakati wote kutilia maanani hali na mazingira yaliyomo katika vifungu vilivyomo kwenye Maandiko. Neno, 'hali' linamaanisha 'pamoja na maeneo ya mazingira.' Ni muhimu kutazama kile kilicho mbele ya maneno yale tunayosoma, au kilichokuwa kikiendelea wakati funzo lile lilipokuwa likitolewa, na kile kufuatacho baada ya mafunzo au tukio hilo ambalo tunajifunza juu yake katika kifungu cha Maandiko. Utangulizi na hali iliyokuwepo hapo mbeleni itatuwezesha kutafsiri kifungu ambacho tunajifunza.

Mwishoni mwa sura ya nne ya kitabu cha Mathayo, tunapata maelezo ya Mathayo ya utangulizi wa lile funzo kuu. Tunasoma kwamba Yesu aliwaponya watu wagonjwa ambao walikuwa wamesafiri mwendo mrefu kutoka nchi na miji mingi, hili wapate kuponywa. (Mathayo 4:23-5:1).

Huku Yesu akiwaponya makutano hao, watu walikuwa wamekusanyika kumzunguka kando mwa ufuo wa bahari ya Galilaya. Alikaribisha baadhi ya wanafunzi wake kukutana naye juu ya milima aiyopanda kutoka bahari ya Galilaya (Marko 3:13). Jambo hii iligawanya watu katika vikundi viwili; huko chini ya mlima walikuwepo wale waliokuwa sehemu ya matatizo. Ilhali huko juu walikuwa pamoja na Yesu waliokuwa sehemu ya kutatuwa na kuitoa jawabu. Sura ile ya tano, ya sita ni jibu na suluhisho. Sura ya saba ya Injili ya Mathayo ni nakala ya mjadala mkuu ambao Yesu alihutubu katika mazingira ya aina hii.

Naitaja hali na mazingira ya mafunzo haya makuu kama, 'faragha ya kwanza ya Kikristo.' Wakati Yesu alipouongoza mkutano huu, changa moto aliyotupa lilikuwa, 'Je! Wewe ni sehemu ya shida au u sehemu ya suluhisho?' Katika faragaha hiyo, Yesu alichagua wanafunzi kuwa sehemu ya suluhisho na jibu lake kwa wale ambao bado walikuwa wangali sehemu ya shida.

Yesu alikuwa akihudumia wagonjwa huku akiifahamu kwamba katika mwili, akiwa kama mtu mmoja, kwa hakika hangeweza kutatua matatizo yao peke Yake, ingawa alikuwa Mungu katika umbo la mwanadamu, Mwanawe Mungu. Hivyo basi, alifanya uchunguzi. Kisha akaongoza faragha ya kwanza ya Kikristo. Kulingana na Marko, kushiriki katika faragha hiyo kulikuwa kwa njia ya mwaliko peke yake (Marko 3:13).

Katika sura hiyo ya saba, tunasoma kwamba Yesu alitamatisha faragha hiyo kwa mwaliko mkuu. Ninashawishika kwamba wakati alipofanya mwaliko huo, alikuwa pamoja na wale kumi na wawili ambao walipokea mwaliko Wake. Msingi wa ushawishi wangu umo juu ya kweli kwamba, baada ya Yesu kushuka juu ya mlima ule, aliwapa Agizo wale mitume na kumi

na wawili. Naamini kwamba Yesu alikuwa akiwachagua mitume Wake kumi na wawili katika faragha hiyo ya kwanza ya Kikristo.

Yaliyomo Katika Ujumbe

Yesu alianza ujumbe kwa kufundisha wanafunzi Wake kuhusu tabia za kuvutia zinazofahamika kama 'sifa za heri', ambazo zingewafanya kuwa sehemu ya suluhisho Lake kwa shida zilizomo chini ya mlima (5:3-12). Tabia hizi zinaelezea mawazo na nia ya mwanafunzi wa Yesu. Kulingana na Yesu, njia ambayo sisi hutazama vitu inaweza kuleta utofauti uliopo kati ya maisha yaliyojaa mwangaza na yale yaliyojaa giza (Mathayo 5:22.23).

Sifa Za Heri: Baadhi Ya Yaliyomo

Sifa hizi nane ndio ujumbe, na yale mengine yote yaliyomo katika mafundisho haya ni matumizi ya ujumbe huu. Baadhi ya walimu na wahubiri wazuri hutumia asilimia ndogo ya mafunzo au mahubiri yao wakiuleta ukweli wanaotaka kuhubiri, pamoja na sehemu ya asilimia kuu ya wakati wao wakihubiri ukweli ambao Alikuwa akihubiri katika (sifa za heri), akionyesha na kutekeleza siza hizo.

Hali na mazingira ya ujumbe huu inatuonyesha pingamizi iliyopo katika kufanyika mfuasi wa Kristo, yaani Mkristo. Sifa hizi za heri zenye kuvutia zinaonyesha maadili yanayohitajika kuwa Mkristo. Mifano minne inayofuatia sifa hizi za heri - chumvi, nuru, mji, na taa - inaeleza changa moto iliyopo wakati sifa za Ukristo zinapokumbana na desturi na mila za kidunia. Hoja kuu ni, 'Je! Wewe ni sehemu ya shida, au u sehemu ya suluhisho la Yesu? Je! Wewe ni mmoja wa jibu au ungali ukiukiza maswali?'

Kuna 'msitari wa kugawanya na wa kiroho' katika kufikiria sifa za heri ya nne na ya tano. Kote katika Maandiko, kuna mfumo unaoibuka wakati Mungu anawachagua viongozi kwa kazi Yake. Wale viongozi walio na ufahamu wa 'ushuhuda wa kumwendea Mungu' na 'ushuhuda wa kwenda kwa niaba ya Mungu.' Wao wana ushuhuda wenye maana ya kumwendea Mungu kabla ya kuwa na matunda ya kwenda kwa niaba Yake. Wao ni waabudu wa Mungu kabla ya kuwa wafanyi kazi Wake. Nne kati ya sifa za heri za kwanza zinaonyesha tabia ambazo mtu hujifunza wakati amwendeapo Mungu, ilhali sehemu ya pili inatuonyesha tabia ambazo ni lazima tujifunze wakati tunapoenda kwa niaba ya Mungu.

Karama inaweza kuendelezwa katika upweke, ilhali tabia ni lazima iendelezwe kwenye kijito cha ubinadamu, au wakati tuko katika uhusiano na watu. Sifa nne za kwanza huendelezwa juu ya mlima, au kile Yesu atakachoeleza hapo baadaye kama ujuzi wetu katika 'chumba kidogo' pamoja na Mungu (Mathayo 6:6). Tunaweza kujifunza na kupalilia zile sifa za heri nne za kwanza katika uhusiano wa kibinafsi na Mungu, lakini fungu lile la pili ni lazima zipaliliwe na kujifunza katika uhusiano wetu na watu wengine.

Sifa hizi pia zinagawanyika katika fungu nne maradufu: Maskini wa roho; wenye huzuni; wenye upole; wenye njaa na kiu ya haki; wenye rehema; wenye moyo safi; wapatanishi na wenye kuudhiwa. Kila moja ya sifa hizi za heri inaeleza kuhusu hali ya kiroho iliyoangaziwa ambayo ni lazima mwanafunzi wa Yesu kujifunza kabla ya kuwa sehemu ya suluhisho na jibu Lake.

Sifa mbili za kwanza zinamfunza mwanafunzi kusema: 'Sio jambo lile niwezalo kutenda ila lile Awezalo kutenda,' au 'bila Yeye, mimi siwezi lo lote.' Fungu la pili linaleta toba kutoka kwa mwanafunzi: 'Sio jambo ninalotaka, ila ni lile Atakalo kutenda.' Fungu la tatu linawakilisha siri hii ya kiroho: 'Haijalishi mimi ni nani au ni nini, ila Yeye ni nani na nini. Fungu lile la nne linashuhudia matokeo ya sifa za heri kupitia haya: 'Haijalishi kile nilichotenda, bali kile Alichotenda.'

Mwishowe, sifa hizi za heri ni kama kukwea juu ya mlima. Sifa ya kwanza hutupandisha kiasi fulani tu juu ya mlima, nao ya pili hutukweza juu kidongo, upole nao hutukweza robo tatu zaidi juu ya mlima, ilhali njaa na kiu ya haki hutupeleka hadi mwisho wa mlima. Sifa hizi za 'kupanda au kukwea' ndio sifa za kumwendea Mungu.

Kila pumziko hufikia mwisho na wale waliohudhuria ni lazima washuke chini ya mlimani. Wakati mwanafunzi anapokuwa amejazwa na haki ya Mungu, Je! Huwa vipi? Je! Huwa kama wale wafuasi wa sheria, na mafarisayo wenye haki ya kibinafsi? La, tunasoma kwamba wao ni wenye rehema na mioyo safi. Kuwa na rehema na mioyo safi, huanzisha safari yao kushuka chini ya mlima hili kuwa sehemu ya suluhisho la Mungu kwa shida za watu walio na mahitaji. Wakati mwanafunzi anapokuwa mpatanishi ambaye huudhiwa, huwa tunamfahamu kama wale walio chini ya mlima tena pale shida ziliopo.

Sifa Za Heri: Mtazamo Wa Kibinafsi

'Heri Walio Maskini wa roho.'

Kuwa maskini wa roho ndio sifa bora kutuhusu wenyewe. Tabia hii ni ufahamu kwamba hatuwezi kuwa suluhisho la Mungu. Ni lazima tuwe watiifu chini ya mfalme, ambaye Ndiye suluhisho. Hii ndio tabia na hali ya utu wetu wa ndani na ya kwanza ambayo tunahitajika kuwa nayo ikiwa tutakuwa sehemu ya suluhisho kwa mahitaji ya wanadamu, na Kristo ambalo anataka kupitia wanafunzi Wake. Kwa neno moja, hali ya neema inayoelezwa kama umaskini wa roho ni 'unyenyekevu.'

'Heri Wenye Huzuni.'

Sifa ya pili heri ni, '*heri wenye huzuni* (5:4).' Tafsiri sanifu na matumizi ya sifa hii ya pili ni kwamba, hatutafanyika kuwa sehemu ya suluhisho na jibu la Yesu kwa shida ambazo zinawakilishwa na watu hao walio chini ya mlima. Hii ikiwa hatuwezi kuudhiwa. Tafsiri nyingine ya matumizi ya sifa hizi ni kwamba, tunahitajika kuhuzunika wakati tunajifunza kwamba tu maskini wa roho, au kwamba hatuwezi kutenda lo lote bila Yeye.

'Heri wenye Upole.'

Dhana hii kuhusu upole ndiyo yenye kutatanisha zaidi katika Biblia. Hii haimaniishi unyonge, ila kuadibika. Hebu mfikirie farasi ambaye bado hajatiishwa, mwenye nguvu mno - mnyama mwenye nguvu ambaye bado hajawekwa lijamu kwenye midomo yake, au hatamu kichwani mwake, au kuwekwa tandiko la kukaliwa juu yake. Nguvu zake zote hazitawaliki. Wakati yule atajitolea mwishowe na kuwekwa lile lijamu na kukubali kuadibika kwa hitamu na lile tandiko, basi yule mnyama ni mfano bora kuhusu maana ya lile neno la Kibiblia yaani 'upole.'

Yesu alitangaza na kusema kwamba Yeye ni mpole (Mathayo 11:20-30). Alipotoa tangazo hilo, alikuwa akisema jambo lile lile. Akizungumza kuhusu Baba, Alisema*: 'Kwa kuwa Mimi huyatenda yale yote ambayo humpendeza Yeye* (Yohana 8:29) Yesu alikuwa ameikubali nira, au kuadibika chini ya mapenzi ya Babake. Hili ndilo lililomfanya kuwa mpole. Katika sifa hii ya heri, Yesu anafunza kwamba tutakuwa tu sehemu ya suluhisho na jawabu katika ulimwengu huu wakati tutakaposalimu amri 'kutaka kwetu' kwa Mungu, na kukubali adhabu ya mapenzi Yake kwa maisha na huduma zetu zaidi ya tamaa.

'Heri wenye njaa na kiu ya haki.'

Sifa hizi za heri sio kwamba tunahitaji kuwa na njaa na kiu ya furaha, bali ya haki. Hebu tazama mkazo umewekwa wapi katika ujumbe huu juu ya kweli kwamba wanafunzi wake ni lazima wawe haki. La ziada katika sifa hii, Atatangaza baraka juu ya mwanafunzi ambaye ameudhiwa kwa ajili ya haki; na thamani kuu ya wanafunzi inahitajika kuwa haki, ilhali haki ya wanafunzi Wake ni lazima izidi ile ya waandishi na mafarisayo (5:10, 20; 6:33).

'Heri wenye rehema.'

Neno ‘rehema’ linamaanisha, ‘upendo usio na masharti.’ Heri watu wale ambao wamejawa kabisa na upendo usio na masharti, upendo wa Mungu.’ Inawezekana kuwa ndio tafsiri rahisi ya sifa hii. Ikiwa utateremka chini kutoka juu ya mlima na kuwa sehemu ya suluhisho kwa wale ambao wamejeruhiwa, ni lazima ujawe na upendo wa Mungu; kujawa na haki ambayo inalinganishwa na kujawa na upendo wake Mungu.

‘Heri wenye moyo safi.’

Neno ‘safi’ katika sifa hii ya heri kwa hakika linatoka kwa lugha ya Kiyunani ambayo ni ‘kusafisha.’ Tafsiri ya tabia na utu huu ni kwamba, wakati mwanafunzi anapenda kwa upendo usio na masharti wa Mungu, hamu ye yote yenye uchoyo itasafishwa na kuondolewa nje ya moyo wake.

‘Heri Wapatanishi.’

Mpatanishi ni mwenye kuleta amani. Shida kuu iliopo hapo chini ya milima ni kutenganishwa. Shida nyingi walio nazo watu zinatokana na kutengwa kwao na Mungu katika maisha yao. Hii ndiyo sababu Yesu aliwapa changa moto wanafunzi Wake hapo katika mapumziko kwamba wao wawe vyombo vya upatanisho.

Kulingana na Paulo, lengo lake kuu katika huduma lililokuwa na wanafunzi wake Yesu, ni ujumbe na huduma ya upatanisho. Twahitaji kwenda nje na kuwaambia watu: ‘Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu (2 Wakorintho 5:20).’

‘Heri wenye Kuudhiwa.’

Ungefikiri kwamba kulikuwa na watu wenye utu na tabia za sifa za heri za kuvutia katika ulimwengu wetu wa leo. Hata hivyo, tabia ya sifa za heri ya nane inatuambia kwamba wao wanafunzi wa Yesu walioudhiwa kwa tabia zao nzuri.

Mwanafunzi mwenye tabia hizi hukumbana na watu kwa mfumo wa kile wanachohitajika kuwa. Wakati wanapopata ujuzi wa kukumbana, basi wanaweza kutubu tabia na hila zao mbovu na kujifunza jinsi ya kupokea tabia ya sifa za heri, au wanaweza kumvamia mwanafunzi kwa tabia njema. Kwa zaidi ya miaka elfu mbili, wao wamekuwa wakitimiza uchaguzi wao wa pili.

Mjumbe wa upatanisho huenda mahali palipo na pingamizi, ambapo mara mwingi pana hatari kuu. Wanafunzi wa kweli wa Yesu wakati wote - hata siku ya leo – husalimisha maisha yao kwa ajili ya huduma za upatanisho. Wanafunzi wamchao Mungu huchukua huduma zao za upatanisho nyumbani mwao, Makanisani, kwa majirani, darasani na hata kazini mwao.

SURA YA SITA
‘Matumizi Ya Mahubiri’

Yesu alifuata maelezo ya tabia ya utu Wake kwa mifano minne yenye maana kuu ambayo inatuonyesha kile kinachotokea wakati tabia ya utu Wake inapokumbana na desturi na tabia za kidunia. Aliwafunza wanafunzi wake kwamba wao ni Chumvi ya dunia . . . Nuru ya Ulimwengu . . . Na Mji uliojengwa juu ya Mlima na ambao hauwezi kusitirika, au taa kwenye kiango (Mathayo 5:13-16). Mifano hii minne ndio msingi wa matumizi ya ujumbe wake. Hebu tutazame mifano, mmoja baada ya mwingine:

‘Ninyi Ni Chumvi ya Dunia.’

Tafsiri moja dhahiri ya matumizi ya mfano huu linahusu kweli kwamba Chumvi peke yake ndio njia ambayo wangehifadhi nyama siku za zamani. Yesu alikuwa akisema kwamba

ulimwengu humo katika hali ya kuoza kama ilivyo nyama, ilhali wanafunzi wake walikuwa ndio 'Chumvi' ambayo ingehifadhi dunia dhidi ya kupotoka kwa maadili na ufisadi wa kiroho. Lugha ya kwanza inaelezea hivi, 'Wewe na ni wewe peke yenu ndio chumvi ya dunia.'

Tafsiri nyingine ya mfano huu inaweza kuwa hakuna kingine kiwezacho kuishi bila chumvi. Kulingana na tafsiri hii, Yesu alikuwa akiwaambia wanafunzi wake kwamba: Wale watu walio chini ya mlima hawana uhai. Lakini, ikiwa mtaishi kulingana na sifa hizio za heri zenye kuvutia, basi ninyi mtakuwa chombo ambacho kupitia kwake, watu hao watapata uzima.'

'Ninyi Ni Nuru Ya Ulimwengu.'

Wakati Yesu alipotazama yale makutano, jambo lile lililomfanya kuwaonea huruma ni kwamba wao walikuwa kama kondoo asiye na mchungaji. Hawakufahamu kushoto kwa kulia. Na kwa sababu unafahamu kile wao hawafahamu, unakuwa nuru ambayo wanahitaji. Kwa mara nyingine, tafsiri ya Kiyunani inasema, 'Wewe peke yako, ndiwe nuru ya ulimwengu.'

'Taa juu ya kiango.'

Tangu mfano huu, Yesu kwa hakika alikuwa akisema: 'Kabla ya kuokoka kwako na kuwa mmoja wa majibu yangu, ulikuwa kama taa ambayo haijawashwa. Lakini kwa kuwa umeshuhudia 'kuzaliwa upya' na kufanyika kuwa mmoja wa wanafunzi wangu, taa lako limewashwa. Kila wakati ninapowasha taa, nina kiango nilichochagua mwenyewe ambacho juu yake, ningependa kwa mpangilio mkuu kuweka taa ile.' Yesu anasema, 'Ninyi ni taa juu ya kiango chake.'

Mji Juu Ya Mlima

Mfano wa nne ni kuhusu mji ulio juu ya mlima, ambao hauwezi kusitiriwa. Ikiwa tuna tabia za utu wa sifa za heri ndani mwa maisha yetu, ushuhuda wetu kwa Kristo hauwezi kusitirirwa. Hakuna mwanafunzi wa siri wa Kristo.

Konokono Juu Ya Nguzo ya Ua

Je! Umewahi kumwona kobe akiwa juu ya nguzo ya ua? Kila mara kumwonapo kono kono akiwa juu ya nguzo ya ua, kuna jambo moja ambalo unafahamu kwa uhakika kuhusu konokono – kwamba bila shaka kuna mtu aliyempandisha juu, kwani hawezi kukwea juu ya nguzo la ua! Kila mwanafunzi wa Yesu ambaye amewekwa pahali fulani anahitajika kujihisi kama yule konokono akiwa juu ya nguzo la uai. Sote twahitajika kutazama kote; na kutambua kwamba tumewekwa kwa nia pote tulipo duniani, huku tukitilia maanani kuhusu taa juu ya kiango na mfano kuhusu mji ulio juu ya mlima, twahitajika kusema, 'Nipo mahali nilipo kwa kuwa Kristo anayeishi ameniweka kuwa hapo hili kuwa sehemu ya suluhisho kwa shida za ulimwengu wenye mahitaji.'

Matumizi Yanaendelea

Yesu anaendelea katika matumizi ya ujumbe wake katika sehemu iliyo ngumu ya mjadala huu (Mathayo 5:17-48). Anatangulia katika sehemu hii ya matumizi kwa kusema mambo mawili yaliyo muhimu: La kwanza ni kwamba Yeye hakuja hili kuharibu sheria, ila kutimiza sheria ya Mungu. Hali halisi ya jambo la pili ni kwamba, haki ya wanafuzi Wake isipozidi ya waandishi na Mafarisayo, wao kwa hakika bado hawajafahamu mafundisho yake (17-20).

Tambua kwamba katika fungu hili ndefu la Maandiko, katika sura ya tano, Yesu anasema mara sita kwamba, '*mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, . . . Bali Mimi nawaambieni* (Mathayo 5:21-48).' Wakati mwingi Yesu alikuwa akinukuu yale yaliyokuwa yamenenwa, hakumnukuu Musa ila Waandishi pamoja na Mafarisayo. Alikuwa akinukuu mambo yale waliyokuwa wakifunza, ambayo kwa hakika hayakuwa yale Musa aliyokuwa

akifunza, wala Neno la Mungu. Wakati anapogusia kitu ambacho Musa alifundisha, anafanya hivyo kwa kutokubaliana na jinsi wao walivyo mtafsiri Musa.

Kina halisi cha mafunzo haya ni: 'Yale yote ninayofundisha yakubaliana nao Neno la Mungu. Hata hivyo, mafunzo yangu hayakubaliani na desturi za Waandishi na Mafarisayo.' Katika sehemu hii kuu ya mjadala, Yesu alikabiliana na mafunzo ya hawa viongozi wa kidini. Ukabiliano wake kwa mafunzo na thamani zao uliendelea hadi wakati walipotambua kwamba hawangeweza kuishi pamoja Naye, hivyo wakamsulubisha.

Kusudi La Maandiko

Tofauti kuu kati ya jinsi Yesu na wale viongozi wa kidini walivyotafsiri na kutekeleza yale Maandiko ilikuwa kwamba, kabla ya kuitekeleza sheria ya Mungu katika maisha ya watu, Yesu aliipitisha katika kioo pembe tatu (ambacho hutumika kupitishia rangi nyeupe kutoka upande mmoja na kutokea upande mwingine kama rangi nyingi sawa na upinde wa mvua) cha upendo wa Mungu. Wakati waandishi pamoja na Mafarisayo walipofunza sheria ya Mungu, hawakufahamu wala kukumbuka sababu au kusudi la Sheria wakati ilipotolewa kwa Musa mlimani Sinai - ambayo ilikuwa ni kwa ajili ya wema wakijamii kwa watu wa Mungu.

Sheria ya Mungu ilikuwa dhihirisho la upendo Wake kwa watu Wake. Ni dhahiri, kwamba Yesu hakuwahi kupoteza kusudi hili la Maandiko. Hii ndiyo sababu Yesu awapa changa moto kujifunza na kutokusahau, wakati watakaposhuka kwenye makutano yaliyokuwa chini ya mlimani. Alikuwa akiwafundza wanafunzi wake kwamba ni lazima wafahamu jinsi ya kuitekeleza sheria ya Mungu katika maisha ya watu Wake ikiwa watakuwa nuru ya ulimwengu.

Haki Ya Uhusiano (21-48)

Baada ya kusema mambo hayo kuhusu umuhimu wa Maandiko katika maisha ya mwanafunzi, Yesu anawaonyesha jinsi ya kutekeleza mafunzo ya uhusiano huo katika maisha yao. Uhusiano wa kwanza ambao Yeye anazungumzia ni ule wa ndugu, au kati ya wanafunzi wengine. Ni jambo la kutiliwa maanani kumsikia Akifundisha kwamba wakati mwingi, Mungu hapewi fursa na thamani ya kwanza, ila 'ndugu yako kwanza, kissha Mungu.' Huku kutilia mkazo thamani hii kwa tuonyesha ukuu na udhamini ambao Yesu anaweka katika uhusiano wetu na waumini wenzetu. Hatuwezi kuvuta ulimwengu upande wetu kama tukipotezana moja kwa mwingine.

Aliwafunza jinsi ya kushirikiana na maadui zao. Tunaishi katika ulimwengu wenye mashindano mengi. Adui wetu ndiye mshindani wetu, au mpinzani wetu (25, 26). Yeye alikuwa na maneno kuhusu uhusiano wao na wanawake (27-30). (Na kwa sababu hapakuwa na mwongozo kuhusu jinsi ya kushirikiana nao, hivyo basi tunaweza kukubaliana kwamba huu ulikuwa mkutano wa wanaume peke yao wa mapumziko.) Wengi hutatanishwa na ufahamu wa mafunzo haya. Hakuwa akifunza kwamba kufikiria kuhusu usherati kulikuwa kukilinganishwa hasa na kitendo chenyewe cha usherati. Mwongozo kwetu ulikuwa kwamba tushinde vita viliopo katika jaribio wakati yahusikana na kutazama na kuwa katika mawazo yetu.

Baadaye, Yesu alizungumzia kuhusu uhusiano wao pamoja na wake zao (31-32). Alifundisha kwamba uhusiano kati yao na wake zao ulikuwa wa daima au milele. Hebu yahusishe mafunz haya kwa yale aliyofunza kuhusu uhusiano wao na wake. Sababu mmoja kuu ya kuzuka kwa talaka siku ya leo ni uzinzi. Wakati kunapokuwa na kuzuka kwa talaka, jamii huvunjika pamoja na watoto kuteseka. Uchungu mwingi pamoja na mateseko yaliyomo 'huko chini ya mlima' ni kwa sababu wanaume wanashindwa katika vita vyao nalo jaribio ambalo Yesu aligusia katika msitari wa (27-30).

Pia walishauriwa wasije wakafuatiliza maneno yao kwa kiapo, jinsi Mafarisayo walivyotenda. Wakati wanaposema 'ndio', wanahitaji kumaanisha ndio, na wakati wanaposema, 'hapana', wahitaji kumaanisha hapana. Wao hawahitaji tu kuwa watu wa Neno (Biblia), bali ni watu wenye kumaanisha Neno lao wenyewe (33-37).

Uadilifu Mkuu (38-48)

Yesu alimalizia kifungu kuhusu matumizi kwa kutupa uadilifu mkuu wa mafunzo yake. Yale Yesu anayofunza katika mistari hii ya mwisho yanawakilisha kiwango kikuu cha uadilifu katika dini ye yote. Funzo hili lilikuwa lenye sababu kuu katika vifo vya mitume na imekuwa hivyo hivyo kwa mamilioni ya wanafunzi kote katika historia ya Kanisa. Mistari hii pia inajulikana kuwa ndiyo gumu sana katika mafunzo ya Yesu. Mbili kati ya misemo yake iliyo gumu ni kwamba hatufai kutolipiza kisasi wakati watu wanapotutendea uovu, ilhali tunahitaji kuwapenda maadui zetu.

Kumbuka kwamba, Yesu hakufunza maadili haya huko chini ya mlima palipokuwa na mchanganyiko wa watu wengi. Wanafunzi wake ndio walichukua msimamo wa kumfuata, hata kufa kwa ajili Yake (Luka 9:23-25; 14:25-35). Alikuwa amedhihirisha wazi kabisa kwa wale waliokuwa wamekiri kuwa wanafunzi wake, kwamba iliwabidi kubeba msalaba huku wakimfuata. Wakati Yesu aliposema, 'msipigane na uovu,' na kwamba, 'mwapende maadui zenu,' alikuwa akiwaambia ni wapi, wakati gani, jinsi gani na ni kwa sababu gani aliwataka wafe.

Katika 'vita vitakatifu' mnamo mwaka wa 1220, *Francis Wa Assisi* alikuwa akihudumia Mturuki mmoja aliyekuwa amejeruhiwa. Mpiga vita moja akiwa juu ya farasi alimtazama *Francis* akiwa na yule Mturuki na kusema, 'huyo Mturuki akipona majeraha yake, kwa hakika, atakuua.' Naye *Francis* akajibu, 'Naam basi, kabla ya kunitendea hivyo, kwa hakika atakuwa ameufahamu upendo wa Kristo!'

Moyo wa kifungu hiki ni swali ambalo Yesu aliuliza, 'Ni yapi unayotenda kuliko mengine? (47).' Kote katika ujumbe huu, kwa hakika Yesu anafundisha kuwa, 'Wewe kama mwanafunzi inakubidi kuwa tofauti.' Tafsiri moja inaelezea swali la Yesu hivi: 'Ikiwa unawapenda wale wanaokupenda, basi unatekeleza neema ipi? Hakuna neema katika kuwapenda wale ambao tayari wanakupenda.'

Kanisa la Agano Jipya lilikuwa na neema ambayo walipokea siku ya Pentekoste (Matendo 2). Neema ile iliwapa watu wa Kanisa hilo uwezo wa kuwa tofauti. Ni lazima tuombe kwa neema wakati tunapotekeleza maadili haya makuu ya Yesu katika uhusiano wetu na maadui zetu.

SURA YA SABA
'Mitazamo Mitatu Ya Kuishi'

Wakati Yesu alipofunza kuhusu tabia za kuvutia, Aliwapa wanafunzi wake changa moto kutazama ndani ya vina vya utu; na kutilia maanani mfumo wa nia ambazo zilikuwa zikiongoza maisha yao. Katika fungu ndefu la Maandiko lililofuatia sifa za heri, Aliwapa changa moto kutazama kote na kutekeleza sifa hiyo katika katika uhusiano wao ulio muhimu sana. Wakati wanafunzi wake waliohudhuria mkutano wa faragha huko mlimani waliposikia jinsi sifa hizi zinavyotekelezwa katika maisha yao, hasa baina yao na maadui, walikuwa tayari zaidi kwa mtazamo wa tatu juu ya jinsi ya kuishi ambao Yesu alishiriki nao.

Tunapoanza kusoma sura ya sita katika kitabu cha Mathayo, tunaona kwamba Yesu aliwaambia wanafunzi wake kutazama juu na kutafakari thamani na nidhamu ya wanafunzi wa kweli. (Neno 'maongozi' na 'mwanafunzi' yanatokana na shina moja). Alishiriki nao maongozi tatu ya kiroho na kufundisha kwamba maongozi hayo ni lazima yatumika katika maisha yao.

Mafarisayo walikuwa na haki ambayo ilikuwa ya kuwazungukia, au kwamba walitekeleza mambo kwa sababu ya sifa kukubalika na watu wengine. Yesu aliwapa changa moto wanafunzi Wake wawe na haki ambayo ilitekeleza ya juu, au iliyokubalika na Mungu. Haya ndio baadhi ya vile alivyomaanisha wakati alipofunza kwamba haki ya wanafunzi wake yanahitajika kuzidi ya Waandishi na Mafarisayo (5:20).

Maongozi Ya Kutoa (1-4)

Maongozi ya kwanza ya kiroho ambayo Yesu anafundisha ni uwakili. Hali ya kiroho yetu pamoja na wema wake huhusiana na tabia ya uaminifu wetu kwa maongozi haya. Matoleo yetu yanahitaji kuelekea juu, au kumwelekea Mungu wala sio kuwafurahisha watu. Ikiwa tunamtolea Mungu, hatuhitaji ye yote kufahamu kile tunachotoa.

Maongozi Ya Maombi - Mawasiliano Na Mungu (5-15)

Huwezi kuwapenda maadui zako, au kuwa sehemu ya jawabu la Kristo katika maisha ya watu ambao bado ni sehemu ya shida, ikiwa haufahamu jinsi ya kuomba. Kwa hakika, huwezi hata kutatua matatizo yako mwenyewe ikiwa hufahamu jinsi ya kuomba. Hii ndio sababu aliwaonyesha na kuwafunza wanafunzi Wake kuhusu maongozi ya maombi.

Jambo kuu katika mafunzo yake kuhusu maombi ni kwamba, ni lazima tuhakikishe kwamba tunazungumza na Mungu wakati tunaomba. Yesu alifundisha kwamba ikiwa unahitaji kuhakikisha kwamba tunazungumza na Mungu wakati tunapooomba, baso tunastahili kuingia katika chumba cha ndani (au pahali pa siri) na kufunga mlango. Kwa kuwa hakuna mtu ye yote wa kumpendeza ila Mungu, maombi yaliyo katika chumba cha ndani ni bora kuliko yale yaliyo mbele za umati kulingana na Yesu. Alihahidi kwamba Mungu wetu, ambaye yumo katika mahali pa faragha, ataheshimu na kukutana na maombi yetu yaliyo ya kweli na ya faragha.

Katika hali hii, Anatupa funzo kuu ambalo ulimwengu huu umewahi kupokea kuhusu jinsi ya kuomba. Funzo hili linaitwa, ‘maombi ya wanafunzi.’ Kuha maombezi saba katika ombi hili. Baada ya kumtaja Mungu kama Baba yetu wa mbinguni, kuna maombezi matatu ya Kiungu: Jina lako, Ufalme wako, na mapenzi Yako. Baadaye, tunahitaji kuomba ‘tupe sisi.’

Kupitia maombezi haya matatu ya Kiungu, tunaomba, ‘Mungu kwanza.’ Maana ya maombi sio kumwendea Mungu ukiwa na orodha ya haja na kumtuma Mungu kutimiza mahitaji hayo. Tunahitaji kuja kwa Mungu katika chumba chetu cha ndani tukiwa na moyo ulio wazi na kumwomba Mungu atutumie hili kutekeleza mahitaji Yake. Punde tunapokuwa na thamani hiyo pahali panapohitajika, basi hapo ndipo tunahitaji kuomba maombi yetu ya kibinafsi. Maombi ya kibinafsi ni haya: ‘Tupe sisi, tusamehe sisi, tuongoze sisi, pamoja na utuokoe sisi.’

Ombi la kwanza la kibinafsi ni, ‘Utupe <u>leo</u> <u>riziki</u> yetu (11).’ Riziki yetu maanake ni yale tunayohitaji. Riziki ambayo tunaiomba ni ya siku ya ‘leo.’ Kisha, tunahitaji kuomba, ‘utusamehe (12).’ Yesu hafunzi kwamba kusamehewa kwetu kunategemea kweli kwamba tunawasamehe wengine. Sisi husameheana kwa kuwa tumesamehewa. Je! Inawezekana vipi kutokuwasamehe wengine ilhali sisi tumesamehewa sana? Lakini tutakuwa na ushuhuda wa msamaha ikiwa tutatekeleza msamaha, kulingana na Yesu.

Ombi la kibinafsi lifuatalo ni, ‘usitutie majaribuni (13).’ Ombi hili kwa hakika ni: ‘Baba, ukiongoza hatua zangu, nami natafuata mwongozo wako, mimi sitakumbana na jaribu.’

Ombi la nne ni, ‘utuokoe na yule mwovu (13).’ Tunafunzwa kumalizia maombi yetu kwa njia ile ile ambayo tulianza nayo kwa kusema ‘Mungu kwanza.’ Tunamalizia kwa kuthibitisha, ‘uwezo wa kujibu maombi yetu yatatoka kwako wakati wote, kwa hivyo matokeo yake (Ufalme) yatakuwa yako, na utukufu utakujia wakati wote.’

Maongozi Ya Kufunga (16-18)

Kama ilivyo kutoa na kuomba, Yesu alifundisha kwamba maongozi ya kiroho ya kufunga ni lazima yaelekezwe juu (16-18). Kufunga ni ujumbe wa Mungu pamoja nasi, kuwa tudhamini yale yaliyo ya kiroho kuliko yale ya mwili. Kulingana na Yesu, kufunga kunadhirisha ukweli wa maombi Yetu. Kuna miujiza ambayo haiwezi kuonekana isipokuwa kwa maombi mengi na kufunga. (Mathayo 17:21).

Maongozi Ya Thamani Za Juu (19-34)

Yesu baadaye, anafundisha ju ya maongozi ya thamani za mbinguni (19-34). Katika kifungu hiki, anaeleza sababu nyingine ya kuteseka kwa wale waliomo humo chini ya mlima. Watu huteseka kwa sababu hawana na thamani za kiroho. Hili wanafunzi wake wawe sehemu

ya suluhisho Lake na jibu kwa watu ambao wangali ni sehemu ya shida, ni lazima wawe na thamani za Kristo za mbinguni na za kiroho.

Kuna hazina huko mbinguni, sawa na humu duniani. Wanafunzi Wake hawahitaji kuweka hazina zao humu duniani ambako thamani yake hupungua na huwa katika hatari za kuibiwa. Wanahitaji kuweka hazina zao huko mbinguni ambako thamani yake haipungui wala haiwezi kuibwa. Yesu anawaambia kwa uwazi mwingi kile wanachohitaji kufahamu kama thamani yao ya kweli. Tafsiri nyepesi ya muhtasari wa mafunzo haya katika siku ya leo inawezekana kuwa: 'Ikiwa unataka kufahamu thamani zako ni zipi, tazama nyuma uone ni wapi umetumia mali yako na utazame kwenye kalenda au takwimu yako ya tarehe ya miaka mitano iliyopita nawe utaona jinsi umetumia muda wako.'

Moyo wako upo pale hazina yako ipo, na ikiwa unataka kufahamu hazina zako ni zipi, basi jiulize mwenyewe maswali haya: 'Je! Unatumia mali na wakati wako vipi? Unafanya nini mchana kutwa? Unataka kupata nini mchana kutwa? Unafedheheshwa na nini mchana kutwa?' Ikiwa utakagua mambo yale utendayo, pamoja na matarajio yako, fedheha zako, basi utatilia mkazo thamani zako.

Anamalizia mjadala juu wa thamani zielekeayo juu kwa kufunza wanafunzi wake kwamba thamani zao na za kipekee ni lazima ziwe ufalme wa Mungu pamoja na haki Yake - kile anachowaonyesha kuwa ni chema. Ikiwa walio na njaa na kiu ya haki watafanya umuhimu wa kipekee wa thamani hizi, basi naye Mungu atawabariki kwa kila kitu ambacho wanahitaji ikiwa watamfanya pamoja na Ufalme Wake kuwa wa Kwanza.

Tazama Ndani (7:1-5)

Tunaposoma sura ya saba ya Mathayo, tunatambua kwamba Yesu anamalizia mkutano wake wa faragha. Baada ya kuwapa changa moto kutazama ndani, kando na juu, anawashauri watazame ndani na kujihoji wenyewe. Akitumia mfano wenye ucheshi, anafundisha kwamba hatustahili kutazama vibanzi vilivyo machoni mwa ndugu zetu ilhali machoni mwetu kuna boriti. Ni lazima tujitazame ndani na kumwuliza Mungu tujihukumu wenyewe kabla ya kuwasaidia wengine. Hivyo basi, ni lazima tufanye uamuzi wa kujitazama ndani na kutoa boriti liliopo ndani mwa macho yetu kabla ya kuwahudumia watu wengine. Yesu anatuambia tusiwe wakosoaji na wanafiki.

Tazama Juu (7:3-5)

Yesu anaendelea kumalizia mafunzo yake kwa kuwakaribisha wale walisikiza mafunzo hayo kufanya uamuzi na kutazama juu. Anafikisha mafunzo hayo mahali pa uamuzi kwa kuwakaribisha wanafunzi hawa kutazama juu na kwa subira – 'Ombeni, tatuteni, bisheni wakati wote. Anafuatisha kwa kifungu hiki cha ahadi hizi tatu: Kila aombaye hupokea, naye atafutaye huona; naye abishaye, mwishowe hujipata amesimama mbele ya mlango uliofunguliwa (Luka 11:9-13).

Tazama Kando (7:12)

Ikiwa wale waliomsikiza wamo tayari kushuka kutoka juu ya mlima, Yesu anawakaribisha kufanya uamuzi kutazama kila upande. Funzo hili ndilo linalotajwa kama, 'mwongozo wa thamani kuu.' Msitari huu mfupi ndio muhtasari wa mafunzo ya Yesu na Biblia nzima kuhusu uadilifu katika uhusiano.

Changa moto kuu katika mafunzo haya ni: 'Ikiwa unataka kuwa chumvi na nuru ambayo watu wa ulimwengu wanahitaji, jiweke mwenyewe mahali panapostahili. Kisha, jiulize hivi: 'Kama ungalikuwa yule mtu, je! Ungemtaka mwanafunzi ambaye amesikia yale uliyosikia hapo juu mlimani kuyafanya?' Ukipata jibu kwa swali hilo, basi litende! Hilo ndilo funzo lililopo katika Biblia kuhusu uhusiano wa wanadamu. Basi cho chote mtakacho kutendewa na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo.'

Kwa matumizi, jiweke mwenyewe mahali pa mwenzio katika ndoa, watoto, wazazi, ndugu wachanga, pamoja na ndugu waumini. Fanya kulingana na funzo hili kwa watu hao ambao maisha yao yanakaribiana na maisha yako. Kama ungelikuwa watu hao, ni kipi ungelipenda kutenda?

Hakikisha kwamba umefanya kulingana na mafunzo haya kwa wale ambao hawajakuja katika imani ya Yesu Kristo; ambao bado hawajakuwa na ushuhuda wa wokovu au baraka ya wokovu. Kisha uliza, 'ikiwa ningekuwa yule mtu, ni lipi ambalo ningependa mwanafunzi wa Yesu Kristo mwenye tabia hizi kutenda?' Baada ya kupata jibu kwa swali lako, litende kwa kuwa hiyo ndio 'Agizo Kuu' la ushuhuda.

Mwaliko (7:13-27)

Wakati Yesu alipoanza faragha hilo, mwaliko wake ulikuwa, 'Je! Wewe ni sehemu ya shida au u sehemu ya jibu? Mwishoni mwa mafunzo, Yesu anawapa changa moto lile alilotoa hapo mwanzoni - ila wakati huu wale wanaosikia mwito huu tayari wamekiri kwamba wanataka kuwa sehemu ya suluhisho. Anapomaliza faragha hilo, mwaliko wake ni, 'utakuwa suluhisho la aina gani?'

Kumalizia mwaliko Wake, Yesu alimalizia faragha hilo kwa kusema: 'Kuna wanafunzi wa aina mbili - wengi na wachache, wasio wa kweli na wa kweli, ambao husema tu na wale hutenda. Wengi hufikiria kwamba kuna njia rahisi kuwa suluhisho au jibu. Hawafanyiki kuwa sehemu ya suluhisho. Hawafanyiki kuwa sehemu ya suluhisho Langu. Ila, walio wachache hutambua kwamba kuwa chumvi ya dunia na nuru ya ulimwengu huanza katika lango jembamba ambalo linafuatiwa na maongozi na maisha magumu ya wanafunzi. Je! Wewe utakuwa sehemu ya walio wengi, au walio wachache? Je! Utakuwa miongoni mwa wasio wa kweli au wanafunzi wa kweli ambao kwa hakika hufanyika kuwa sehemu ya suluhisho Langu? Je! Utakuwa mmoja wa wale husema tu au wale hutenda niliyofunza juu ya mlima huu?'

Mfano huu mkuu ambao Yesu anamalizia nao mjadala huu unatuonyesha aina mbili ya wanafunzi walio tayari kushuka kutoka juu ya mlima. Yesu anatupa picha ya nyumba mbili (maisha), moja imejengwa juu ya mwamba (mwanafunzi ambaye anatii mafunzo ya Yesu) na nyingine ambayo imejengwa juu ya changarawe (mwanafunzi ambaye hatii mafunzo Yake). Wote wamesikia mafunzo haya, lakini mmoja wao - yule mpumbavu – hafanyi kulingana na yale aliyosikia. Yule mwingine amesikia na kutenda kulingana na mafunzo yote. Kumalizia huku kuna uwezo mkuu hivi kwamba tofauti kati ya wanafunzi hao wawili ni kile wanachotenda kulingana na ufahamu wao (Mathayo 7:24-27).'

Kwa kuwa tayari umekagua mafunzo haya makuu, basi utakuwa mwanafunzi wa aina gani kwa Yesu? Ni yapi ambayo utatenda kuhusu kile unachojua?

SURA YA NANE
'Mwito Wa Wale Waliojitolea'

Hatuna hesabu kamili ya wanafunzi wale ambao walihudhuria faragha ya kwanza ya Kikristo. Jinsi vile tayari nimetambua, punde baada ya Yesu kumaliza mafunzo yake huko mlimani kwa mwaliko, Aliwaagiza wale wanafunzi kumi na wawili kuwa mitume. Ni dhahiri kwamba Yesu aliwachagua hawa mitume hapo katika faragha ya Kikristo kisha akawaagiza kushiriki katika huduma yake – na kuwa sehemu ya mpango Wake mwafaka wa kuwafikia watu kote ulimwenguni kwa wokovu ambao alileta ulimwenguni.

Jinsi nilivyouliza hapo awali, kama ungefahamu kuwa ulikuwa na miaka mitatu tu kuishi na kufanya kazi yako, ni lipi ambalo ungetenda? Yesu kwa hakika, alifahamu kwamba alikuwa na miaka mitatu na hii ndio sababu aliwaajibisha na kuwashirikisha mitume katika hamu yake kufikia ulimwengu kwa wokovu. Wanafunzi wake kwa uaminifu walieneza Habari Njema nyakati

zote za maisha yao. Karne tano baada ya Yesu kuwaagiza hivyo, hakuna mtu angeweza kupata kazi katika Milki ya Warumi isipokuwa akiri kwamba alikuwa Mkristo. Kwa njia hiyo, ni lazima tuwe waaminifu kufikia ulimwengu wetu kwa ajili ya Kristo tunapotangaza Injili hiyo ulimwenguni ambapo tunaishi.

Kutana Na Mitume Kumi Na Wawili

Yesu alitumia usiku kucha katika maombi kabla ya kuwaagiza hawa mitume kumi na wawili (Luka 6:12, 13). Mitume wanne wa kwanza ambao wanatajwa katika Mathayo ni kundi la ndugu wawili wawili; Petro na Andrea, Yakobo Na Yohana. Hawa ndugu wanne walikuwa katika biashara ya uvuvi pamoja.

Filipo na Bartolomayo kila mara wanatajwa kwa pamoja, jinsi ilivyo Tomaso na Mathayo. Filipo alikuwa ni mwana-biashara ambaye biashara yake ilikuwa ni ya farasi au ya usafiri. Yawezekana kwamba kama ni katika siku ya leo yeye angelikuwa katika biashara ya magari. Tunapolinganisha orodha zao wanafunzi katika Injili tofauti, sisi twakubaliana kwamba huyu Bathalomeyo alikuwa akijulikana pia kama Nathanieli.

Tomaso alikuwa ni msomi mwenye akili ya kuulizauliza. Siku yaleo twamtaja mtu kama yule kuwa ni “Tomaso mwenye shuku.” Mathayo alikuwa ni mtoza ushuru, mlimwengu, aliyeokota ushuru kwa niaba yao Warumi kutoka kwao watu Wayahudi wa jamii yake, hii ilimaanisha kwamba yeye alikuwa ni kama msaliti kwao watu wake. Utatambua kwamba Injili zawataja ‘Watenda maovu na watoza ushuru.’ Hii haimaanisha kwamba hawa watoza ushuru hawakuwa ni wenye dhambi. Hii yamaanisha kwamba hawa watoza ushuru walikuwa ni wenye dhabmbi katika daraja la kipekee! Watu wa Kiyahudi kwa hakika waliwachukia mno hawa watoza ushuru. Ni jambo la kuvutia kuona kwamba Yesu alimchagua mtoza ushuru kuwa ni mmoja wao kumi na wawili.

Majina manne ya mwisho ni majina ambayo yamenukuliwa mara nyingine katika orodha ya kumi na wawili. Kwa mfano, kulikuwepo na Simoni mwingine, kando na Simoni Petro. Simoni huyu mwingine aliitwa ‘Mkananiyos ua “Mwenye juhudi.” Hii yamaanisha kwamba yeye alikuwa ni kinyume chake mtu kama vile Mathayo. Yeye alikuwa katika lile kundi lao watu wenye Juhudi mno, na ambao walikuwa ni wapiganaji vita dhidi ya utawala wao Warumi, hata ingawa Wayahudi walikuwa wamo chini ya utawala wao Warumi. Siku yaleo twawataja watu kama hawa kuwa ni wana-mapinduzi. Wasomi waamini kwamba watatu au wanne miongoni mwao mitume walikuwa ni wa Zelote au wana-mapinduzi.

Wakati wote nimekuwa ni kuliwaza jambo hili, Je! Huyu Simoni mwana-mapinduzi na yule Mathayo mtoza ushuru waliyazungumzia mambo yapi - kama kuwa wao waliongeleshana kwa vyo vyote vile - huku walipokuwa wakitembea naye Yesu katika Galilaya, Yudea, Yerusalemu na hata huko Samaria. Waweza kuona tukio lilikuwepo hapo wakati ambapo Yesu alipomwambia yule Mathayo mtoza ushuru, na Simoni mwana-mapinduzi kuoshana miguu yao na kupendana wao moja kwa mwingine. (Yohana 13:34,35).

Kulikuwepo naye Yakobo mwingine katika orodha ile yao kumi na wawili, ambaye aitwaye “Yakobo mwana wa Alfayo.” Huyu Yakobo pia atajwa kama “Yakobo aliyepungua,” ambayo maana yake yawezekana kuwa kwamba yeye alikuwa ni mfupi au alikuwa ni kijana (Marko 15:40). Walikuwepo watu wengine wawili katika orodha ile wenye kulishiriki jina Yuda. Yupo Yuda ndugu yake Yakobo,” na ambaye pia aitwaye “Thadayo” au “Lebaya,” na Yuda Iscarioti ambaye aliye msaliti Yesu.

Mitume hawa walikuwa waihubiri Injili na waudhihirisha Ufalme wake Mungu kwa kupitia ishara na maajabu. Ilikuwa wao wawaponye wagonjwa, wawatakase wenye ukoma, wawatoe mapepo na kuwafufua wafu. Walikuwa wahubiri na kuitoa Injili bila ya malipo ye yote na bila ya kumuuliza mtu cho chote kile, huku wakimtumainia Mungu kwa kukutana nayo mahitaji yao yote. Walikuwa waishi kwa imani.”

Yesu aliwaonya hawa mitume kwamba wao hawatapokelewa vyema. Yeye aliwaonya wao kwamba: “Angalieni Mimi nawatuma kama kondoo kati yao mbwa-mwitu.” (Mathayo 10:16)

Yeye alikuwa akiwaonya hivi: ulimwengu hautawatakieni ninyi mema wakati ambapo mtakapoutii mwito wangu na kuutekeleza mpango wangu makhususi." Hii ingali ni kweli hata katika siku ya leo.

Jukumu

Utatunukiwa ufahamu na kubarikiwa ikiwa utayajibu haya maswali sita kuwahusu hawa mitume kumi na wawili ambao Yesu alikuwa nao kwa muda wa miaka mitatu Yake katika huduma kwao watu, na ambao yeye aliwakabithia jukumu kuu lake kwa ulimwengu huu:

Alikuwa akitenda kitu gani alipokutana naye Yesu?

Yeye alibadilika kwa njia ipi kama tukio la kweli kwamba yeye alikutana naye Yesu?

Yeye alikuwa wapi wakati alipokufa?

Alikuwa akifanya nini alipokufa?

Kutokana na yale ambayo wewe waweza kujifundisha, kutoka katika maandiko na toka katika sehemu nyingine, yeye alikufa kwa njia gani?

Ni kwa sababu gani Yesu alimchagua huyu mtu ili awe mtume?

Yesu alikuwa amewauliza wao kujitolea kukuu wakati ambapo yeye aliwapa ule mwito mkuu juu ya mlima kwa sababu Yeye aliwafahamu hawa mitume walikuwa watapitia katika dhiki na kufa kwa ajili Yake. Ni kiwango kipi ulicho nacho cha kujitolea kwake Yesu Kristo? Je! Wewe ni mwanafunzi wake wa kweli? Je! Wewe upo tayari kujitolea kwake Yesu jinsi ambavyo tunao mfano wa kujitolea kwa maisha yao mitume?

SURA YA KUMI
"Hadithi Zake Yesu Zenye Mafumbo Zilizomo Katika Mathayo"

Sura ile ya kumi na tatu ya Mathayo ndiyo sura kuu yenye hadithi za mafumbo katika Injili hii. Hadithi yenye mafumbo ni ile ambayo "Yarushwa kando na" kweli ambayo mtu yule anajaribu kuifunza. Yesu alikuwa ni mjuzi mno katika kuzitumia hizi hadithi zenye mafumbo.

Kulikuwepo nao wakati katika Huduma yake ambapo Yeye alizitumia hadithi zenye mafumbo katika kufunza kwake. Sababu mmoja wapo ilikuwa ni kwamba Yeye hangelitiwa korokoroni kwa kuzitoa hadithi ndogo ndogo ambazo siyo rahisi kuzielewa. Ni wale tu ambao walikuwa naye Roho Mtakatifu ndio wangeliyaelewa yale mafumbo Yake. Sura ile ya kumi na tatu ya Mathayo ni hadithi kuu mno ya mafumbo, katika sura hii. Na kwa kuwa huu ni ukaguzi tu wa Injili ya Mathayo, nitakuwa nao wakati tu wa kuufanya utangulizi kwa dhana ya hadithi ile yenye mafumbo na kuitoa mifano michache kuhusu hadithi za mafumbo ambazo Yesu alizifundisha.

Yesu aanza kwa hadithi ya fumbo lake Mpanzi. Mkulima aenda na kuzipanda mbegu katika shamba lake. Yule mkulima anazitoa mbegu toka katika mfuko wake na kuzitawanya. Baadhi ya zile mbegu, zalianguka kando ya njia, pale ambapo watu walikuwa wamepitia na kupafanya kuwa ni pagumu. Na hivyo basi zile mbegu zilielea juu ya udongo ule. Zile mbegu hazikuweza kupenya ndani ya ule udongo, na hivyo basi ndege walikuja na kuzila zile mbegu.

Nyingine ya zile mbegu zake yule mpanzi ziluangukia udongo usio mwingi penye miamba, nazo zile mbegu zikaanza kuitoa mizizi yake katika udongo ule juu ya miamba ile, lakini mizizi ile haikupenye na kuwa na kina kwenye ile miamba hivyo basi wakati jua lilipozuka ziliungua na kunyauka wala hazikuyazaa matunda kwa kuwa hazikuwa nayo mizizi.

Mbegu zingine nazo ziliangukia pale penye udongo ulio bora; na ambao wenye kina kikuu na unyevu-nyevu nazo zile mbegu zikaitoa mizizi yake. Lakini wakati ile mimea ilipoanza kukua, ilikumbana nayo miiba , ambayo iliisonga ile mimea hivi kwamba haikuweza kuyazalisha matunda.

Mbegu zile za mwisho zake yule mpanzi ziliuangukia udongo ambao ni mzuri. Na ambao hauna nayo matatizo ye yote yale chini mwake au juu ya ule udongo. Mbegu zile ziliyazaa matunda; baadhi yake thelathini-, nyingine sitini- na nyinginezo mia moja toka kwa ile mbegu iliyopandwa.

Tunapoisoma hii hadithi yenye mifano twakubaliana kwamba hii hadithi ingelipewa jina hili, “Hadithi yake Mpanzi.” Lakini tunapoizoma ile hadithi kwa umakinifu zaidi, yamkini twaweza kuipa jina hili, “Hadithi ya Mbegu.” Kwa kuwa “Mbegu ni Neno,” hadithi hii ni mafunzo makubwa mno kulihusu Neno lake Mungu pamoja nayo baadhi ya mambo yale yanayo husika wakati Neno lake Mungu lahubiriwa au kufunzwa. “Jiagalieni basi jinsi msikiavyo” (Luka 8:18).

Baada yake Yesu kufundisha kuhusu hii hadithi yenye mafumbo, Yeye alikuwa peke yake pamoja nao mitume, wao walimwuliza Yeye kuhusu tafsiri ya mafumbo yale naye akawapa wao tafsiri yake. Akawaambia wao kwamba mbegu ile ambayo yule mpanzi aliyoipanda ndilo Neno lake Mungu nao ule udongo wa namna mbali mbali uliwakisha njia nne ambazo kwazo watu hulipokea Neno lake Mungu.

Tunaposoma ile tafsiri yake Bwana kuihusu ile hadithi, sisi twatambua kwamba jina bora kwa hadithi ile labda ingilekuwa ni, “Hadithi Kuhusu Udongo.” Tunapotafakari kweli kwamba mkazo mkuu wa ile hadithi ni juu ya vile ambavyo watu wanalipokea Neno Lake Mungu, sisi twatambua kwamba yamkini jina bora zaidi lingelikuwa ni, “Njia Nne Zakulisikiliza neno Lake Mungu,” kwa kuwa hadithi hii ya mafumbo yatupatia maelezo manne kuhusu jinsi ambavyo watu hulipokea Neno Lake Mungu wakati linapo hubiriwa au kufunzwa.

Wakati ambapo Neno linapotolewa, mtu yule wa kwanza hata halielewi lile Neno; mawazo yao au ule ufahamu wao ni mgumu na hujapenywa bado na hivyo basi wao hawayazai matunda ye yote yale.

Mtu yule wa pili analielewa lile Neno. Ufahamu wao unapenywa, lakini udongo wao siyo mwingi wa kulishikilia lile Neno, na hivyo basi miamba iliyo chini huizuia ile mizizi ya ile mbegu kupenya kina chake hii nayo yawakilisha kile ambacho Yesu akitaja mahala pengine kuwa ni “Moyo uliyo mgumu.” Hii yamaanisha kwamba mapenzi yao hayajapenyezwa na pia kwamba kujitolea kwao ni kwa juu juu. Wao wanaliamini Neno, na wakati ambapo wakumbana nayo dhiki au mateso, wao huanguka mara moja, na hivyo basi wao hawayazai matunda.

Mtu yule wa tatu yeye hashindwi nalo jambo lo lote lililo chini ya udongo au katika maisha yake, kama ulivyo ufahamu wa mawazo yake au kule kujitolea kwa hiari na mapenzi yao. Wao washidwa nazo nguvu zilizopo juu ya ule udongo au nje ya maisha yao, kama vile ule udanganyifu wa mali na utajiri, pamoja nazo anasa zake. Wao pia waweza kushindwa nazo “Fedheha za ulimwengu huu,” au na kule kufedheheshwa nao utajiri walio nao au ule ambao hawana nao. Katika hadithi ile, pingamizi hizi ni kwekwe ambazo huisonga mimea ambayo neno lingelitaka kukua katika udongo wa maisha yao. Mtu huyu wa tatu pia hayazai matunda.

Twaweza kusema kwamba yule mtu wa kwanza ameivaa “Kofia ngumu,” ya kiroho. Yule wa pili anao moyo mgumu, naye yule wa tatu yeye amefedheheshwa kwayo maamuzi magumu aliyo nayo.

Ule udongo wa nne ni picha ya ambavyo Yesu angelitutakia sisi sote kulipokea Neno lake Mungu wakati tunapolisikia. Hamna cho chote kile chini ya ule udongo au juu yake ambalo ni pingamizi la kukua au kuyazaa matunda. Hii ni picha yake mtu ambaye huufanya waamuzi kwamba hamna cho chote kile kilichoko maishani mwake, kama vile ule ufahamu wao au mapenzi yao yenye ukaidi yatawazuia wao kutokuyazaa matunda. Pia wao huufanya uamuzi kwamba hamna cho chote kile katika ulimwengu huu kilicho katika namna ya uwezo uliopo nje ya maisha yao utawazuia wao katika kuyatimiliza makusudio yake Mungu kwa kuwapa wao Neno Lake Mungu.

Na kama ambavyo Luka anavyoeleza, “Baada ya kulipokea Neno kwa ukweli na wema wa moyo, yeye Huliweka hilo,” na jambo hili humfanya yeye kuwa mtu mwenye kuyazaa

matunda (Luka 8:15). Luka pia aeleza hali ya asili ya hadithi hii kuu ya mafumbo kwa maneno haya: “Jiangalieni basi jinsi msikiavyo;” (Luka 8:18)

Kweli ya hadithi hii kuu ya mafumbo ni dhahiri kwake ye yote yule anayelifundisha au kulihubiri Neno Lake Mungu. Wakati Neno lake Mungu linapohubiriwa, hawa watu wanne wapo pale wakati wote naye mhubiri au mwalimu mwenye upambanuzi aweza kukuonyesha wewe.

Wale wote ambao husikia na kuyafunza Maandiko wahitajika kufikiria zaidi kuhusu hadithi hii ya mafumbo wakati ambapo wao wanalisikiliza au kulifunza Neno Lake Mungu. Kwanza kabisa, ni lazima tuutizame ule udongo wetu binafsi. Ni udongo wa namna gani uliopo katika mioyo yetu? Je! Sisi tupo tayari kuliruhusu Neno lake Mungu kuyazaa matunda? Je! Sisi ni wenye kuyazaa matunda mengi, kama vile asili mia moja (100%) au ni matunda machache kama vile asili mia thelathini (30%)? La pili, wale ambao hufundisha wahitajika kutilia maanani kabisa wa kweli nzito kwamba mafunzo au mahubiri ya Neno Lake Mungu yatakuwa bila ya mazao ikiwa wale ambao wanafunzwa hawaielewi maana ya Neno lile ambalo wao wanalisikiliza.

Twahitajika kufahamu zaidi kwamba mafunzo au mahubiri yetu yatakuwa nayo mazao, ikiwa tu mapenzi yao wale ambao sisi twawafunza yatapenywa. Wakati ambapo sisi tunafundisha ni lazima, basi kufunza kwa urahisi hivi kwamba tuupenye ule ufahamu wao. Ni lazima kwamba, kwa njia ya Maombi kuyaleta mafunzo na mahubiri yetu kuufikia uamuzi kwamba Roho Mtakatifu apate kuyapenya mapenzi nao uamuzi wao ambao huyasikiliza mafunzo na mahubiri Yetu.

Sisi hatupewi changa moto ye yote ile katika hadithi hii kuu ya mafumbo ili kuwa ni watu “Wasanifu Wa Bibilia” ambao waifahamu Bibilia, bali kwao wanafunzi wake Bwana waliojitolea ili kulitenda Neno lake Mungu ambalo limepenya katika ufahamu na yale mapenzi yao. Hivyo basi, ni lazima sisi tusikie, tufunze, na kulihubiri Neno, huku tukiomba kwamba Roho Mtakatifu akapate kuyafunua macho ya kiroho yao wale ambao watusikiliza sisi ili kwamba wakapate kufahamu na kulitii Neno Lake Mungu. Twahitajika kumuomba Yeye apate kutupatia sisi, na wale ambao watusikiliza sisi kipawa cha imani, na “Mapenzi yale ya kulitenda” Neno, ili kwamba lile Neno lipate kuwa nayo mazao (Yohana 7:17; Philipians 2:13).

Ni lazima pia tukamtegemee Mungu kutuwezesha sisi, pamoja nao wale wanaotusikiliza sisi, kuzishinda nguvu zote zile zilizomo ulimwenguni huu, na ambazo zaweza kukifanya cho chote kile ambacho kimo chini ya uweza wao kuona kwamba kule kusikia kwetu, na yale mahubiri na mafunzo ya Neno kuwa hayazai lo lote. Ni Mungu peke yake awezaye kuyafanya haya mambo. Hii ndio sababu wakati tunaposoma, au kufundisha, au kulihudumu neno, ni lazima iwe ni, “Maombi na huduma ile ya Neno”; haya mawili ni yalazima kuambatana. (Matendo 6:4)

Hadithi Ya Mafumbo Kuhusu Ngano Na Magugu (Mathayo 13: 24-30; 36-42)

Hadithi hii kuu na iliyo fupi, pamoja nayo tafsiri yake, ni funzo mmoja wapo la muhimu lake Yesu kwa sababu ni jawabu kwa lile swala ambalo limekumbana nao wanatheolojia na wana falsafa tangia wakati ule ambapo taratibu hizi za falsafa na theolojia zilipoanzia. Swala ni hili, “Uovu ulitoka wapi?” au kwa maneno mengine, “Twawezaji kuukiri ule uwepo wa uovu katika ulimwengu ambao umeumbwa na kudumishwa naye Mungu wa upendo na Mweza yote?”

Jibu lake Yesu kwa njia ya hadithi ya mafumbo ni hili, “Adui wangu ndiye aliyeyatenda haya, wakati watu walipokuwa wakilala.” Mwanzo wa dhambi watajwa kutoka “Kwake adui yangu,” na pia kule kupuzilia kwake mwanadamu. Fafanuzi hii yake Yesu yamkini yawezekana kwamba ilimvuvia mtu yule ambaye aliyaandika haya maneno; “Yale yote ambayo yahitajika ili kwamba uovu uwe nao ushindi juu ya wema ni kule kutokutenda cho chote kile kwa watu wema.”

Katika fumbo hili, “mbegu” sizo maneno yake Mungu yaliyoanguka juu ya udongo wa mioyoni mwa maisha yao wanadamu, ila ni wana wa ufalme waliopandwa katika udongo wa ulimwengu huu. Labda hatuwezi kufahamu, lakini pale tunapoukubali ukweli wa uovu, changa moto yafanyika kuwa: “Ni jambo lipi ambalo tutalifanya kuhusu hii shida? “Konde au shamba ni ulimwengu,” kulingana naye Yesu, na hii yatufanya sisi kufikiria kuhusu mzigo ambao wakati mwingi yeye aliuzungumzia. Yeye aliwapa wanafunzi wake kuomba kwamba Mungu akapate kuwatuma watenda kazi katika shamba au konde lile kwa kuwa mavuno ni tayari bali watenda kazi ni wachache (Mathew 9:37, 38).

John Wesley alifahamu na kuushiriki mtizamo huu wake Kristo wakati alipotangaza, ‘Ulimwengu ndio mtaa wangu!’ Hebu tusije tukaupoteza mtizamo wa kweli kwamba “Ulimwengu ndio konde,” na sio tu eneo lile letu tu katika lile konde. Twahitajika tuwe nao ule mtizamo wa ulimwengu mzima tunapoikubali ile changa moto kwamba wema na uovu upo ulimwenguni.

Fumbo la Mbegu ya Haradali na ile Chachu (Mathayo 13: 31-33)

fumbo hizi mbili zimetimilika katika historia yote ya Kanisa. Fumbo hizi fupi zafundisha kwamba ufalme ambao Yesu aliuzungumzia ungelianza ukiwa ni mdogo, kama jinsi ambavyo mbegu ya haradali inavyofanyika na kuwa ni mti mkubwa, na kile kipimo cha chachu ambacho huwekwa katika unga uliokandwa wakati mkate unapotengezwa na hivyo kuchanganyikana katika ule mkate mzima na kuufanya kukua mkubwa.

Lakini hata hivyo, katika mafumbo haya mawili, Yesu anatabiri kwamba huu ufalme utakuzwa kwa njia isiyo ya kawaida kama vile ambavyo ukuzi wa ile mbegu ya haradali na ushawishi kama ule ulio kama chachu inavyoufanya mkate. Miaka elfu mbili baadaye, sehemu kubwa ulimwenguni huihesabu tariki yake kulingana na kabla ya maisha yake pamoja nao ushawishi huu wake Mtu alyeitwa Yesu.

Ile ya kanuni ya chachu na ile mbegu ya haradali ingali yatenda kazi hata katika siku ya leo. Tunapoutilia maanani ule ukuzi wa kanisa, hata katika sehemu ambapo ipo dhiki na mateso, sisi twaona kule kutimilizwa kwa fumbo hizi mbili zilizo fupi.

Kama ilivyo katika lile fumbo lake yule Mpanzi, ndege ambao walikuja na kuyafanya makao katika matawi ya mti huu, ni ishara zisizo njema ambazo zauonyesha umati uliochanganyikana wao wale ambao sio sehemu ya ufalme ila kwamba wao wakiri kuwa wao ni sehemu ya ufalme. Msukumo mkuu wa funzo hili, naamini ni kule kukua na ule ushindi mkuu wa mwisho wa ufalme pamoja nao ushawishi wao wana wa kiume na wa kike katika ule ufalme.

Hata ingawa wakati mwingi chachu huuwakilisha uovu katika sehemu nyingine katika Maandiko, hiyo haiwakilishi uovu katika fumbo hili ila ule uwepo nao ushawishi wa Ufalme ule katika ulimwengu huu. Ikiwa haiwakilishi uovu hapa, hivyo basi fumbo hili lafundisha ule ufisadi mkuu katika ufalme, na ambao hauambatani nao mkazo ambao upo katika Maandiko kuhusu ule ushindi mkuu na wa mwisho juu ya wema dhidi ya ule uovu, juu yake Mungu kinyume chake Shetani, na juu ya Kristo aliyemshinda kama Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana.

Fumbo la Hazina na Lulu (Mathayo 13:44-46)

Fumbo hizi mbili na zilizo fupi na ambazo kwa hakika zaabatana pamoja, ni picha yenye kuvutia ya kufurahika, kujitolea kikamilifu kwake Mfalme na Ufalme Wake. Wao wasema nasi hivi, “Ikiwa Yesu Kristo ni kitu cho chote kile kwako wewe, basi, ni hakika kwamba Yesu ndio kila kitu kwako wewe, kwa kuwa hadi wakati ambapo Yesu Kristo amekuwa ni kila kitu kwako, hakika ni kwamba Yesu Kristo siyo kitu cho chote kile kwako.”

Hatujauona ufalme ambao Yesu anaoufundisha, hadi wakati ambapo sisi tutakapo uona huu ufalme kuwa ndio jambo kuu kabisa ambalo tumewahi kuliona. Ufalme wa mbinguni wastahili kushangiliwaa na kujitolea kabisa kwetu sisi. Mafumbo haya yatufundisha sisi kwamba kwa hakika hatutaweza kufahamu na kuudhamini ufalme hadi wakati ambapo kwa ile

furaha kuu tutajitolea wenyewe kukiuza kila kitu tulicho nacho na kujitolea kile chote ambacho ni sisi kwake Mfalme ambaye ni mtawala wa ufalme huu.

Fumbo la Msamaha (Mathayo 18:15-35)

Hali na mazingara ya fumbo hili kuu ni ule mwongozo kuhusu kuwasamehe ndugu zetu. Petro alikuwa ameliuliza swali hili kwamba ni mara ngapi ambazo yeye atakikana kumsamehe ndugu ambaye aliyemkosea yeye. Hali na desturi ya siku ile ilikuwa kwamba waweza kumsamehe nduguyo kwa mara saba, na yawezekana ndio sababu yake Petro agusia numbari hii saba. Fundisho lake Yesu lilikuwa kwamba msamaha wako kwake nduguyo wahitajika usiwe nacho kipimo. Maana kamili ni "Saba mara saba, na mara sabini,' ambayo ni hesabu isiyo na mwisho katika siku moja. Na dhana yake kwa msimamo huu wadhihirishwa nalo fumbo lifuatalo.

Deni kubwa iliyosamehewa yawakilisha msamaha wa dhambi zetu zote wakati ambapo tulioupata ujuzi wa wokovu. Wokovu wetu wahusika na kule kuondolewa kwa 'deni' zetu zote au msamaha wa kila dhambi ile ambayo tushawahi kuitenda.

Fumbo hili ni mfululizo muhimu kwa lile Ombi lao Wanafunzi. Yesu alitufundisha sisi kuomba kwamba madeni yetu yasamehewe kama ambavyo sisi twawasamehe wadeni wetu. Alifuatilia ule mwongozo wa maombi kwa shauri kuu, kwamba ikiwa sisi hatutawasamehe wadeni wetu, Baba yetu hatatusamehe sisi makosa yetu.

Fumbo hili la jumulisha kwa shauri hilo hilo. Injili ya wokovu yatangaza, "Wakati ambapo Yesu alipokufa juu ya msalabani, Yeye aliilipa deni ambayo haikuwa ni yake, kwa kuwa sisi tulikuwa ni wadeni ambao hawangeliweza kuilipia ile deni.' Sisi hatusamehewi kwa kuwa sisi twawasamehe wengine. Sisi twaonyesha kwamba kwa hakika sisi twaamini kuwa sisi tumesamehewa kwa kuwa sisi huwasamehe watu wengine. Kwa hakika yatubidi sisi kuwasamehe watu wengine, kama ambavyo Mungu kwa niaba yake Kristo alivyotusamehe sisi (Waefeso 4:32, Wakolosai 3:12, 13)

Fumbo kuzihusu Hati Za Utumishi (Mathayo 21:23, 28-31)

Hii ni mmoja wapo ya mafumbo yenye kuvutia mno yake Yesu. Wakati ambapo Mungu alifanyika na kuwa ni Mwanadamu na kuja katika ulimwengu huu, ambao huzidhamini mno Hati za utumishi, Yeye alifanyika kuwa ni Mtu asiye nayo Hati ya utumishi isipokuwa ule utendaji wake. Mmoja wapo ya vitofautisho vikuu kati yake Yesu na wale Mafarisayo ulikuwa kwamba Yeye alitilia dhamana kuu juu ya utendaji na dhamana ndogo kwa ule usanifu wenye misingi yake kwenye hati za kuhitimu masomo. Wao walikuwa na dhamana zilizo kinyume. Sehemu kuu ya ubishi imo katikati ya hili fumbo dogo.

Wana wawili waliopo katika fumbo hili walidai kitu kimoja, lakini wakakitenda kitu kingine. Usanifu wao ulikuwa basi, ni ule usio nayo maana ye yote, nao ule utendaji wao ulikuwa ndio Hati kuu ya kukubaliwa kwao. Tendo lililokuwa dhahiri kwao viongozi wa kidini lilikuwa kwamba Yesu na Yohana Mbatizaji hawakuwa nazo Hati za namna ambayo ilikubaliwa nao ulimwengu wa kidini wa wakati ule. Na kulingana na ule usanifu wao, wao hawakuwa wakijitambulisha wenyewe kama wana wake Mungu waliokuwa wakitenda kazi katika bustani yake Mungu; lakini kulingana nao utendaji wao katika lile bustani, na wao walikuwa wakiitenda kazi yake Baba.

Na kwa upande mwingine, wale viongozi wa kidini walikuwa wao ni wasanifu wasio nao utendaji. Na kwa mavazi yao, na mitego ilyopo katika desturi pamoja nayo ile ishara ya daraja lao la kidini, wao walikuwa wakikiri kuwa wao ni wana wake Mungu katika kazini shambani mwake Mungu. Kulingana nao utendaji wao, hata hivyo, ilikuwa ni dhahiri kwamba wao hawakuwa wakiitenda kazi yake Baba.

Wakati Yesu alipoulizwa Hati yake ya Kukubaliwa, Haya ndio yaliyokuwa majibu yake makuu. Utendaji wake ulikuwa ndio Hati Yake, nasi twajidanganya wenyewe, hadi wakati ambapo tutakapotambua kwamba utendaji wetu, na wala sio ule usanifu wetu wakisomo, kuwa

ndio Hati yetu ya kweli inayokubalika. Yakisiwa kwamba wapo Wachungaji au makasisi Mililioni mbili katika ulimwengu huu wa leo na wachache mno kama vile laki moja hivi wamehitimu katika shule ya Bibilia au Seminari na kuipokea Shahada. Hii yamaanisha kwamba wengi wao wachugaji katika ulimwengu huu wa leo wahitaji kulisikia hili fumbo lake Yesu. Yafuatayo ni kama maelezo juu ya fumbo hili kuu.

Maisha Ya Kipeke Yake Mtu Moja

"Kuzaliwa katika kijiji kisichotambulikana, Yeye alikuwa ni mwanawe mwanamke aliye wa kawaida kabisa. Aliajiriwa katika karakana au kiwanda kidogo cha useremala hadi alipoufikia umri wa miaka thelathini, na halafu kwa miaka mitatu Yeye alisafiri kote nchini, na kusimama kwa kitambo hivi kwamba angeliweza kuwazungumzia na kuwasikiliza watu, na kuwasaidia pale ambapo pange-liwezekana.

"Yeye hakukiandika kitabu, Yeye hakuwa nayo rekodi ya wimbo (Sahani ya Gramafoni) iliyovutia mno, Yeye hakukihudhuria Chuo, Yeye hakushindania kiti cha uongozi katika jamii, Yeye hakuwa nayo jamii yake mwenyewe, wala hakuwa nayo nyumba. Yeye hakuyatenda mambo yale ambayo huambatana nao ukuu. Yeye hakuwa nayo Hati ya kutambulikana isipokuwa Yeye mwenyewe.

"Alipokuwa nao umri wa thelathini na tatu, wimbi la maoni yao watu lilikuwa kinyume chake, nao marafiki zake wote wakamkataa. Wakati aliposhikwa, ni wachache mno ambao waliotaka cho chote kile kuhusiana naye. Baada ya hukumu isiyo kuwa ya haki, yeye aliuawa nayo serekali pamoja nao wezi waliokiri. Na ni kwa sababu ya ukarimu wake rafikiye akampatia kaburi lake pale ambapo angelizikwa.

"Haya yote yalitukia karne ishirini zilizo pita, na hata hivyo Yeye ndiye kiongozi mkuu katika kizazi cha binadamu, na mfano mkuu wa Upendo. Na hivyo silo jambo la kutia chumvi kusema kwamba majeshi yote ambayo yamewahi kuwapo, na wanabaharia ambao wamewahi kuyatia matanga yao, na viongozi wote ambao wamewahi kutawala, nao wafalme wote ambao wamewahi kuumiliki ulimwengu, wote kama wakiwekwa pamoja hawajawahi kuyagusa maisha yao watu duniani kama ambavyo yale Maisha ya Kipekee yake Mtu Mmoja." (Fred Bock)

Fumbo La Jumapili Ya Mtende (Mathayo 21:33-46)

Mamilioni yao watu wafahamu kwamba Yesu alipanda juu ya mwana-punda akiingia huko Yerusalemu katika Jumapili ya Kwanza ya Mtende. Je! Umewahi kuyasoma yale ambayo Yesu aliyoyatenda alipomshuka yule mwana-punda? Yesu aliifuma hali na mazingara ya utangulizi wa fumbo hili lenye uwezo mkuu na lenye kushangaza kwa kuulani Mtini na kulitakasa Hekalu. Fumbo hili liliuleta ule mjadala kati yake Yesu nao hawa viongozi wa kidini katika kilele cha uhasimu au uadui mkuu.

Yaliyomo katika fumbo hili ni picha yake Mungu akiwatuma manabii (watumishi) wake kuyapokea matunda ya ufalme. Wakati hawa watumishi wafanyiwa aibu yule mwana wa mwenye lile shamba atumwa ili kuyapokea matunda ya shamba lake Babaye. Yule mwenye lile shamba adhania kwamba wao watamheshimu yule mwanawe, lakini badala ya kumheshimu yeye, wao wamuua yeye! Na kwa hakika, Yesu ndiye Mwana katika fumbo hili, nao hawa viongozi wa kidini wamo katika ule mpango wa Kumuua Yeye wakati ule ule.

Baadhi ya maneno mazito ambayo Yesu amewahi kuyanena yapatikana katika mwishoni mwa sura hii ndefu wakati ambapo Yesu autumia mfano wa kusisimua ili kuwajumuisha viongozi wa dini ya Kiyahudi. Yeye autumia huu mfano ili kuwajulisha viongozi wa kidini, kwamba kwa kuwa wao hawakuwa wakiyazaa matunda ya Ufalme, ufalme utachukuliwa toka kwao na kupewa kwao watu wengine ambao watayaleta matunda ya ufalme huo.

Twayaona haya yakitendaka kama vile yalivyonenwa katika kile Kitabu cha Matendo wakati watu walio chaguliwa wake Mungu walifanyika kuwa ni kanisa (Matendo 10, 11). Mfano ambao wafunzwa toka katika fumbo hili ni kwamba wakati watu wake Mungu washindwa

kuuangukia mwamba wa kule kujitolea kwake Kristo na kuupokea ule ujuzi wa hali ya kuvunjika Kwake, na kwa mapenzi yake pamoja na kwa kazi yake, ule mwamba mwishowe huwaangukia juu yao wale na kuwaponda na kuwasaga kama unga.

Katika maandiko, ule mti wa mtini ni ishara ya Israeli. Wakati tunapotambuliza ule mfano ulio hapo mwishoni mwa sura hii kwa kule kuulaani ule mtini, sisi twatambua kwamba Yesu alikuwa akiwaambia wale viongozi wa Israeli kwamba Baba yake Mungu anakifanya kitu kile kile kwa kumpitia Yeye kile ambacho alikitenda kwao watu Waebrania huko nyikani. Sura ile kuu ya kumi na nne katika Kitabu cha Hesabu yahitajika katika fumbo hili lenye kutumaakinisha sisi. Mungu alikuwa kwa subira kuu amejidhitisha kwao wana wa Israeli huko nyikani, na kwa mara kumi, kwa kuipitia miujiza. Yeye aendelea na kutangaza kwamba wao wangeliangamia huko nyikani kwa sababu wao hawangeliewa kuamini na kuivamia Kanani na kuichukua ile Nchi ya Ahadi.

Imo njia ambayo Yesu 'Aliwafuta kazi' wale viongozi wa Kiyahudi wa kidini wakati ambapo Yeye aliuondoa ufalme toka kwao katika ile Jumapili ya Kwanza ya Mitende. Kote katika historia ya kanisa hii Jumapili ya Mitende imetimizwa kwa mara kadha. Yaonekana kwamba Mungu 'Aliyasogeza Makao Makuu' toka kwa kanisa katika sehemu fulani ya ulimwengu ambapo matunda ya ufalme yalikuwa yamekoma kuzalishwa, hadi pale ambapo kanisa lililo kuwa likiyazaa matunda ya Ufalme.

Jinsi Ya Kukaribia Mafumbo Ya Yesu

Kuna mafumbo arobaini na saba katika Injili tatu zinazolingana. Nimechagua baadhi ya mifano michache hili kukujulisha katika eneo hili muhimu ya mafunzo ya Yesu yaliyomo katika Injili ya Mathayo. Nakuhimiza kusoma kwa makini mafunzo haya na kwa undani kabisa. Utakapokuwa ukifanya hivyo, nina mawazo kuhusu jinsi unaweza kukaribia mafumbo haya ambayo nataka kukushauri:

Kumbuka kwamba fumbo ni hadithi ambayo mwalimu hutupa sambamba na ukweli ambao anataka kufunza. Yesu alikuwa mtaalamu mkuu wa mfumo huu wa kufunza. Tunastahili kutafuta kweli kuu ya kila fumbo ambalo Yesu alifundisha kwa kuwa mafumbo Yake huenda sambamba na kweli moja.

Unapojaribu kutafsiri mafumbo ya Yesu, ni jambo la muhimu kufahamu hali na utangulizi wa kila fumbo.Hivyo basi, wakati unaposoma fumbo la Yesu, unahitaji kujiuliza maswali haya: Ni katika hali na utangulizi gani ambao uliokuwepo wakati fumbo hilo lilipotolewa? Fumbo hili lilitolewa wapi? Ni wakati upi ambapo fumbo hili lilitolewa? Fumbo hili lilitolewa katika mazingira, matendo au ushirika na watu wapi hadi kuliongoza hadi kwa hili funzo? Fumbo hili lilikuwa la watu wagapi? Kwa maoni yako, lengo la Yesu kufunza fumbo hili ni lipi? Ni Kweli kuu gani inayoambatana ambayo inaelekezwa kwa hadithi hii. Ikiwa tafsiri ingetolewa na Yesu, kubali tafsiri hiyo. Ikiwa sivyo, kuwa mnyenyekevu kuhusu tafsiri yako. Fumbo inaweza kuwa na tafsiri moja iliyokubalika lakini iwe na matumizi mengi. Hivyo basi, wakati wote jiulize, 'Ni vipi ambavyo Mungu anataka kutumia mfanoi huu katika maisha, jamii, na Kanisa langu?'

SURA YA KUMI
'Mafunzo Ya Yesu Yanathaminiwa Sana Katika Mathayo'

Agizo Kuu Lingine

'Njooni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu

wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangi ni mwepesi (11:28-30).'

Jinsi tulivyoona hapo mwisho wa wa mjadala mkuu wa Yesu, Alipenda kumalizia mafunzo yake kwa wosia na kutoa mwaliko. Huu ni mmoja wa myaliko mikuu Yake. Mwaliko huu unaelekezwa kwa wote ambao wana mizigo mizito, na katika hali ya uchovu huku wakijaribu kubeba mizigo hiyo kwa nguvu zao wenyewe. Mizigo ile inazidi kuwa mikubwa na yenye uchovu ambao hauwezi kuvumiliwa. Mwito huu ni kumjia Kristo, hili kupumzishwa mizigo yao mizito, kisha kupokea pumziko kwa roho zao, na kuvumbua kwamba maisha yaweza kuwa mepesi na mizigo yao myepesi.

Kwa mara ya kwanza, ni kama tu kuja kwake na kupokea pumziko ya mizigo yetu. Lakini, tunavyotilia maanani mwito huu kwa makini zaidi, tunatambua kwamba anatukaribisha tuje na kujifunza. Tumekaribishwa kujifunza kuhusu mzigo Wake, moyo Wake, pamoja na nira Yake.

Hakuna mwanadamu aliyewahi kubeba mzigo mzito kuliko ule Yesu aliobeba hapa ulimwenguni. Hata hivyo, tunamsikia akisema, 'mzigo Wangu ni mwepesi!' Ikiwa tunataka kupata mapumziko kwa mioyo yetu pamoja na raha kutoka kwa mizigo yetu, basi Aliyetufunza kwamba heri ni wale wenye upole, anatukaribisha kujifunza kuhusu unyenyekevu wa moyo pamoja na upole Wake.

Yeye anatukaribisha kujifunza kuhusu nira Yake. Tunakaribishwa kupokea nidhamu ya Yesu Kristo na kufungwa nira pamoja Naye kama wanafunzi Wake. Msingi wa kufahamu mwito huu ni kwa kutilia maanani kile alichomaanisha wakati atakapotukaribisha kuchukuwa 'nira' Yake katika maisha yetu.

Nira sio mzigo, bali ni chombo ambacho hutuwezesha kusafirisha mizigo mizito. Fikiria juu ya gari ambalo huvutwa na fahali likiwa limejaa mizigo mingi. Kisha, fikiria kwamba unamtaka yule fahali kuvuta gari hilo. Basi unaweza kutambua lengo la nira. Fahali hana akili au ufahamu wa kuvuta gari hilo kwa shingo lake, lakini anaweza kuvalishwa nira hili kumwezesha kulivuta gari hilo. Nira ni chombo ambacho humwezesha fahali kutenda jambo ambalo haliwezekani na kuvuta gari hilo.

Kwa hali hiyo, mafunzo pamoja na mashauri ya Yesu ni 'nira' ambayo inatuwezesha kuvuta au kubeba mizigo mikubwa ya maisha. Haya ndio Yesu aliyokuwa akimaanisha wakati alipotushauri kuwa kwa kupokea nira Yake, kutafanya maisha yetu kuwa mepesi kwa sababu tumetiwa nira pamoja Naye.

Mwaliko huu mkuu ni kumjia Kristo. Yeye hatualiki kwenda Kanisani au katika kundi la kujifunza Biblia au pia kundi la usaidizi, wala katika mkutano, au moja wapo ya tamasha ambazo zinatuleta kwake Kristo. Mwito huu ni kumjia Kristo. Yeye anatukaribisha tuje na kuwa na uhusiano pamoja Naye. Pia, anatukaribisha hili tukumbane na maisha jinsi Alivyokumbana nayo. Ikiwa tutatazamia maisha kupitia thamani Zake pamoja na maongozi ya kiroho, basi anatuhahidi kuwa tutapata pumziko na faraja katika mioyo yetu kwa kupumzishwa mizigo yetu mizito, na kwa maisha ambayo sio ya kujilazimisha, yaliyo mepesi kwa sababu tumefungwa nira katika uhusiano pamoja Naye.

Ufalme Unafanyika Kanisa (Mathayo 16:13-23)

Hiki ni kifungu muhimu sana katika Injili kwa sababu huo ndio wakati wa kwanza Yesu anataja neno 'Kanisa.' Pamoja na Yohana Mbatizaji, walianza huduma yao wakiwahubiria watu Habari Njema za ufalme wa Mungu. Juu mlimani na katika mafumbo, alitangaza Injili ya ufalme wa mbinguni, au wa Mungu. Kwa wakati huu, Yesu anatangaza kwamba atalijenga Kanisa Lake na malango ya kuzimu hayataweza kumzuia. Pia anatangaza kwamba atajenga Kanisa Lake juu ya mtume Petro.

Mazingira yaliofuatia tangazo hili ni kwamba, Yesu aliwauliza wanafunzi wake, '*watu humnena Mwana wa Adamu kuwa ni nani?'* naye Petro akajibu, *'Wewe ni Kristo!' Jinsi u*ngamo

la Petro lilivyo muhimu, jibu la Yesu kwa ungamo lake lina umuhimu mkuu. Hili kufafanua zaidi jibu lile, ni kana kwamba Yesu anasema: *'Simoni, wewe si mwerevu vilivyo! Ni baba yangu ambaye amekufunulia wewe! Mimi nitalijenga Kanisa Langu juu ya muijiza kwamba mtu kama wewe angelisema jambo lililo nzuri kama hilo, Petro - kwamba watu walio wa kawaida watayatenda mambo yasio ya kawaida kwa sababu Roho Mtakatifu anakaa ndani mwao. Nguvu za kuzimu hazitalishinda Kanisa, kwa kuwa nguvu zilizo ndani mwenu na nyuma ya Kanisa Langu zitakuwa ni Roho Mtakatifu!'*

Ingawa huu ni mfumo tofauti wa usemi, hatuhitajiki kuliona jambo hili kama ubishi. Je! Yesu alikuwa akijenga ufalme au Kanisa? Sio hili wala lile, lakini ni yote kwa pamoja.Ufalme ni dhihirisho la mapenzi ya Mungu juu ya nchi jinsi ilivyo huko mbinguni. Kanisa litakuwa lile lile wakati litakapofanyika kuwa Lake, likitimiza mapenzi Yake humu duniani.

Fungu hili ni la ajabu kwa sababu wakati Yesu aliposhiriki lengo kuu la huduma Yake kuhusu mauti yake huko Yerusalemu, Petro alimkemea Bwanake! Kisha Yesu akamgeukia yule mtu, ambaye hivi karibuni alikuwa chombo ambacho Mungu alizungumza kupitia, na kumwita 'Shetani.' Yesu anamwambia kwamba anasimama katikati mwa mapenzi ya Mungu, akiyazuia mapenzi ya Mungu wala hadhihirishi mapenzi ya Mungu, ila ya Shetani!

Majibizano haya ya kushangaza kati ya Petro na Yesu ni dhahiri kwamba yanatufunza kwamba tunaweza kuwa watu wa kawaida mume au mke ambaye mambo yasio ya kawaida yanatendeka kwa sababu ya Roho Mtakatifu. Majibizano haya yenye uwezo mkuu pia yanatufunza kinyume cha ukweli huo! Tunaweza kuwa vyombo ambavyo mapenzi ya Mungu yanaweza kuzuiwa kufika humu duniani ilhali ya Shetani yanafika. Jambo hili linaweza kudhihirishwa kupitia yule mtu yamkini tu kwa dakika chache baadaye!

Tunasema Yesu Ni Nani?

Hadithi yinaelezwa kwamba Yesu alirudi usiku wa manane kwenye malango ya Seminari ya thiologia (elimu ya dini). Alibisha malango kwa kupiga kengele na wakati mkuu wa Seminari hiyo alipojibu, Yesu aliuliza, 'Wewe unasema kuwa mimi ni nani?' Naye mkuu wa Seminari akajibu, 'Kwa Nini, Wewe ndiwe kina kikuu cha uwepo wetu. Wewe ndiwe uwezo ambao hutuwezesha kukusudia uhusiano wetu wote!' naye Yesu akasema, 'Mambo gani hayo?' Ni jambo la muhimu kwetu kuwa na jibu bora kwa swali hili ambalo Yesu aliuliza mitume Wake. Tunahitaji kufahamu kwamba Yeye ni Yesu Kristo, Masihi, Mkombozi aliyeahidiwa na Mwokozi wa ulimwengu.

Filosofia Ya Uongozi Wa Yesu (Mathayo 23:1-12)

Kifungu hiki kinatuonyesha filosofia ya Yesu ya mapinduzi kuhusu wokovu. Funzo hili linalingana na funzo Lake la hapo awali wakati alipowaambia kutumikiana mmoja kwa mwingine, jinsi Yeye anavyowatumikia wao wote (Mathayo 20:20-28). Aliwaonyesha na kuwafunza kweli hii wakati alipowatawadha miguu yao kwenye chumba cha orofano (Yohana 13:1-17). Yeye yu sahihi kabisa wakati anawapa mfumo wa uongozi wwa Ufalme (Kanisa) wake, ambao misingi yake ni katika utumishi na unyenyekevu.

Ikiwa tutakuwa makini katika utekelezaji wa filosofia hii ya uongozi kwenye Makanisa yetu ya leo, tutatambua kwamba hakuna kitu cho chote ulimwenguni kinachofanana na Kanisa. Kulingana na funzo hili, na lile ambalo lipo katika Mathayo sura ya ishirini, Kanisa linastahili kuwa jamii ya kipekee ambapo hapatatikani kuwa na 'Juu – Chini' kama ilivyo katika ulimwengu.

Kuna mambo matatu yaliyokatazwa ambayo yanatajwa hapa na Yesu. Katika kuiwasilisha filosofia ya uongozi, anatumia waandishi na mafarisayo hili kuwatayarisha mitume kusikia mambo hayo matatu yaliyokatazwa. Waandishi na Mafarisayo walikuwa kinyume cha yale yote ambayo Yesu aliamini na kufunza katika filosofia au sera Yake ya uongozi. Wao walipenda kutilia mkazo 'Juu-Chini', kana kwamba wao wako 'juu', ilhali wale wengine wako

‘chini.’ Walipenda meza kuu katika karamu, na kusalimiwa katika umati na pia kuitwa ‘Rabi’, ‘Mwalimu’ na ‘Baba.’

Akiwatumia viongozi hawa wa dini kama utangulizi Wake, Yesu anaeleza mambo matatu yaliyokatazwa katika mfumo wa uongozi wa Kanisa Lake. Anatumbia kwamba tusimruhusu mtu Ye yote kutuita ‘Rabi” – ‘Mwalimu Mkuu’ - kwa kuwa tunaye Rabi mmoja, ambaye ni Kristo, nasi sote tuko katika kiwango kimoja, kama ndugu! Katika hali hii, Yesu anatuambia tusimruhusu mtu ye yote kutuita ‘Baba’ au ‘Mwalimu.’ Tafsiri nyingine zinamwita mwalimu huyu ‘kiongozi.’ Sababu ya mwongozo huu ni kwamba, Baba yako ni Mungu, naye Mwalimu au kiongozi ni Kristo nanyi nyote mko katika kiwango kimoja, kama ndugu.

Je! Tunaweza kutekeleza hii filosofia hiii ya uongozi yake Yesu katika mifumo yetu ya uongozi Makanisani leo? Ni vigumu sana kwangu kufahamu kisa na maana cha kutiliwa mkazo ‘Juu – Chini’ katika sehemu fulani za Kanisa siku ya leo. Sababu ya kidunia ya ‘vyeo vya ukuu’, pamoja na mambo yale yanayoambatana na ishara za vyeo na tabaka husema kwamba mtu mmoja ni bora kuliko mwingine, na mwingine yu juu, au anastahili kuliko mwingine. Hali hii imekolea katika mashirika mengi ya Makanisa siku ya leo jinsi ilivyo katika wanajeshi. Yesu anafunza kwamba mfumo wa uongozi wa Kanisa unastahili kuwa tofauti (Mathayo 23:11, 12, Yakobo 2:1-9).

Mahubiri Ya Mlima Wa Mizeituni (Mathayo 24, 25)

Huu ndio mjadala wa Yesu kuhusu kuja Kwake kwa mara ya Pili na mwisho wa ulimwengu. Sawa na mjadala wake katika chumba cha orofani, mjadala huu unaanza kwa majadiliano na huenda kulikuwa nayo mazumgumzo huku mjadala ukiendelea. Yeye pamoja na mitume wanataja baadhi ya mambo makuu kuhusu Hekalu. Naye Yesu anawajibu kwa kutangaza kwamba wakati waja ambapo hapatakuwa na jiwe juu ya lingine katika Hekalu hilo kuu.

Nao mitume wanauliza maswali haya matatu: ‘Mambo haya yatatukia lini? Ishara yake itakuwa ipi? Nayo ishara ya kuja kwako itakuwa ipi?’ kisha ‘ishara ya mwisho wa dunia itakuwa ipi?’ Unaposamo huu mjadala wa Yesu, yaache haya maswali matatu ya mitume na majibu yake kuwa mwongozo wa mjadala huu mkuu kwako.

Kuja kwa pili kwa Kristo sio tukio moja bali ni mfululizo wa matukio mengi. Jinsi ulivyo unabii wa Biblia, changa moto ipo katika kutenganisha tukio ambalo lilitabiriwa kutokea hivi karibuni na lile ambalo limetabiriwa kutokea hapo siku za usoni. Miaka arobaini baada ya mjahubiri haya kufanyika, Warumi waliharibu kabisa Hekalu. Hakukubaki jiwe juu ya lingine. Tukio hilo la kusababisha uharibifu kwa hakika lilikuwa likielezwa katika mahubiri haya.

‘Mambo haya’ yaliyomo katika maswali ya mitume na katika jibu lae Yesu yanahusiana na tukio hilo. ‘Mmoja atanyakuliwa na mwingine ataachwa.’ Haya yanahusu kunyakuliwa kwa Kanisa jinsi mtume Paulo anasemavyo katika (1 Wathesalonike 4:13-17). Dhiki kuu inaambatana na matukio yaliyomo katika kitabu cha Ufunuo ambapo hukumu za mihuri, panda au tarumbeta, na vitasa au bakuli zinatabiri kuhusu dhiki kuu itakayo kuja (Ufunuo 6-19).

Wale mitume waliuliza ishara kwa matukio haya matatu. Yesu anafunza kwamba hakuna mtu ambaye anafahamu wakati matukio haya yatakapotukia, lakini jinsi tunavyoshuhudia ishara za hali ya hewa mbaya zikikaribia, kutakuwepo na ishara za kuja Kwake na za mwisho wa dunia. Baadhi ya ishara hizo ni: vita na tetesi za vita. Tunataja tetesi za vita kuwa ‘vita baridi).’ Mataifa na falme zitapigana. (tunataja vita hivyo kuwa ‘vita vya dunia).’ Njaa, tetemeko za ardhi, kuanguka kwa waumini wengi pia ni baadhi ya ishara hizo. Hivyo basi, tunachukulia mambo haya matatu kwa umuhimu mkuu.

Yeye anatabiri kuja Kwake kutakuwa kwa kushangaza, kama ilivyo mwangaza kutoka kwa umeme juu mawinguni pamoja na ishara hizi zote. Kuja Kwake kutatokea wakati hatutarajii. Hata hivyo, changa moto yake kwetu ni kukesha na kuhakikishiwa kwamba wakati atakaporudi, Atatupata tukiwa tu watumishi Wake waaminifu.

Matumizi kwa mjadala huu uko katika mfumo wa mafumbo matatu yaliyo katika sura ya ishirini na tano. Fumbo la kwanza linatuelekeza kufahamu kwamba hukumu Yake itakuwa juu ya kila chombo ambacho ni kikavu. Mafuta ni ishara ya Roho Mtakatifu katika Biblia. Wale wanawali watano wapumbavu, ambao hawana mafuta katika taa zao ni picha ya wale ambao wamo Kanisani ila wao si watu wa kiroho wakati Yeye arudipo. Changa moto katika fumbo la kwanza ni kwamba, wakati Bwana harusi (Yesu) atakaporudi tena, itakuwa ni kuchelewa kabisa kuwaendea wale ambao huyaleta mafuta (Waumini) hili kuyapata kwa ajili ya taa au vyombo vyao.

Mvuto mkuu wa fumbo la pili ni kwamba, kuja kwake ni hukumu kwa kila mikono iliyo mitupu. Hii ni hadithi inayotambulikana ya talanta. Sote tutaulizwa lile swali ambalo Mungu alilomwuliza Musa*, 'Ni kipi kipo kwenye mkono wako?* (Kutoka 4:2).' Maandiko mengine yanatuambia kwamba kiti cha hukumu cha Kristo kitafuatia mjio wake pili (1 Wakorintho 3: 13-15; 2 Wakorintho 5:10). Fumbo hili linatufunza kuwa mawakili waaminifu kwa yale Mungu ametukabidhi mikononi mwetu.

Fumbo la tatu linatekeleza mjadala huu mkuu kwa kufunza kwamba kuja Kwake kwa pili kutakuwa hukumu kwa kila moyo ulio mtupu -wale ambao hawakuwajali waliokuwa na kiu, njaa, mavazi, wagonjwa, au wale waliomo gerezani. Watu wale ambao Yesu anataja kama 'ndugu zangu' ambao wamo katika dhiki yawezekana kwamba ni wanafunzi ambao wameteseka kwa mahitaji haya huku wakitumikia Agizo Kuu ya Kristo ambayo amekabidhi kwa Kanisa Lake.

SURA YA KUMI NA MOJA
'Matukio Makuu Ya Yesu (Mathayo 26-28)'

Vile sura hizi tatu zinavyosimulia ufufuo na kifo cha Yesu Kristo, pia zinashiriki katika baadhi ya mafunzo na mifano muhimu ya Yesu. Ni katika hali hii ambayo Yesu anabadilisha mfumo wa kimsingi katika ibada ya Kiyahudi ya Pasaka na kuwa mfumo wa msingi kwa Kanisa, ambao unatajwa kama 'Meza ya Bwana' au 'Ushirika Mtakatifu.' Pia, mfumo huo upo katika pingamizi kuu Lake wakati tunapomsikia Yesu akiomba katika bustani la Gethsamane, sala ambalo linafaa kuitwa 'Sala ya Bwana.'

Baada ya ya Ufufuo wake, aliwapa mitume pamoja na wanafunzi Agizo Kuu. Hivyo basi, unapozidi kusoma sura hizi, tilia maanani mfumo wa kimsingi wa ibada ya Kanisa, ombi lenye mfano la Yesu, na Agizo Kuu la Yesu.

Meza Ya Bwana (Mathayo 26:17-35)

Wakati mume na baba anaposafiri mbali na jamii yake na kwa muda mrefu, mara kwa mara picha yake hutolewa na kuwekwa karibu na jamii yake. Picha hii hufanyika kuwa ni ya muhimu kwa jamii hiyo wakati wametenganishwa na baba yao. Wakati anaporudi kutoka safarini, na kujiunga na jamii katika umoja na upendo, kwa mara nyingine hawahitaji picha hiyo tena.

Kuna hali ambapo haya ndio maana ya vile Yesu alivyofanya wakati alipozindua mfumo huu wa ibada. Alifahamu kwamba atasafiri kwa muda mrefu. Hivyo basi, alilipa Kanisa 'picha'Yake mwenyewe, na kusema maneno haya kwetu, *'Nitakapokuwa sipo, ningependa mnikumbuke kwa kutazama picha hii.'*Wakati atakaporudi tena, hatutahitaji picha hiyo, lakini hadi wakati huo; hivi ndivyo amechagulia sisi tuwe tukimkumbuka.

Wakati Yesu alipokutana na mitume katika chumba cha orofani, alifahamu kwamba baadhi yao watamkariri kwa picha za maneno jinsi walivyoandika katika Injili nne. Kutokana na njia hizo, Alifahamu kwamba watafanya kumbukumbu Yake - kwa kufufua wafu, kuponya wagonjwa, kutuliza tufani, kuwapenda wenye dhambi, kuwafunza na kuwaajibisha mitume

wake -Aliwapa picha na kuwaambia, *'Hii ndio njia ambayo nataka kukumbukwa kwayo! Na kila wakati mnapokusanyika pamoja na kumega mkate huu na kunywa kikombe hiki, ninyi mnakikumbuka kifo changu hadi wakati nitakaporudi tena!* (Mathayo 26:26-29, 1 Wakorintho 11: 26).' Meza ya Bwana ni 'picha' Yake mwenyewe ambayo alipatia Kanisa Lake; na huu ndio mwongozo ambao Alipatia Kanisa kuhusu ibada!

Sala Ya Bwana (Mathayo 26:38,39)

Kwa kuwa Yesu hakufanya sala lile alilowafunza wanafunzi wake, hili ndilo sala ambalo linahitajika kuitwa, 'sala ya Bwana,' na linafaa kutiliwa maanani kama mfano wa kuigwa wa maombi kwetu sote. Maneno yenye ufunguo hapa ni, 'Siyo mapenzi yangu, bali mapenzi yako yatendeke!' Kweli hii iko katika Sala ya Wanafunzi. Sala hii pia inatufunza kwamba ni utangamano kati ya mapenzi yetu waumini na ya Mungu – ufahamu wa uwepo wa Mungu ambao unatutangamanisha na mapenzi ya Mungu na matokeo yake huwa sisi kuitwa kulingana na makusudio Yake (Warumi 8:26-28).

Sehemu ya kwanza katika sala hii ya Yesu ni mwongozo na mfano kwetu: 'Baba, ikiwa yawezekana, hebu hiki kikombe ni kiepuke mimi.' Kama wana wa Mungu, wakati wote tuko haki kusali hivyo. Ikiwa utaambiwa, au watu wale unaowapenda wana jambo mbovu linalowajia, una haki na wajibu kusali hivyo. Kwa maelezo mengine, una haki kuomba kwa uponyaji. Lakini kuomba jinsi Yesu alivyosali katika sala hii ya mwongozo, ni lazima umalizie sala hilo kwa kuomba hivi: 'Na isiwe vile ninavyotaka, bali unavyotaka Wewe.'

Watu wengi wanaamini kwamba inaonyesha kutokuwa na imani kwa ombi la uponyaji, kwa kusema, 'Ikiwa ni mapenzi Yako.' Mimi siwezi kuelewa vile watu wanavyoweza kusema hayo wakati ambapo Mwana wa Mungu Mwenyewe alivyoomba hivyo. Ikiwa Yeye hangeomba kwa njia ambayo aliomba kuhusu msalaba, basi hapangekuwa na waokovu kwa ye yote! Wale wote ambao wameokolewa watakuwa na shkurani ya milele, kutokana na ombi hilo la kielelezo kwetu la Yesu. Kulikuwepo na upatanisho au utangamano kati ya mapenzi ya Mungu Baba pamoja na Mapenzi ya Mungu Mwana ambayo matokeo yake yalikuwa wokovu!

Kifo Cha Yesu Kristo (Mathayo 27:11-34)

Wakati Injili hizi tatu za kwanza zinapoeleza kifo cha Yesu Kristo, zina ufasaha mwingi kwa yale yanayonenwa ndani yake. Hazituelezi mambo yenye uchungu wala picha mbaya kuhusu kusulubiwa. Vitabu hivyo vinaeleza tukio hilo mbaya kwa maneno matatu pekee: *'Wao Wakamsulubisha Yeye.'* Tutapokea nuru zaidi kuhusu kifo cha Yesu ikiwa tutatilia maanani maneno haya matatu.

'Wao Wakamsulubisha Yeye!'

Kusulubishwa kulikuwa jambo la ukatili mkuu, ingawa kulikuwa jambo la kawaida ya Warumi kuwahukumu watu. Ingelimchukuwa siku tano au juma nzima kwake yule mtuhumiwa kufa kufuatia kusulubiwa. Raia wa Kirumi hangesulubiwa kwa kwani hukumu ya mauaji ilikuwa ni mateso. Ilitambulikana kama mateso ya kikatili, na kwa kuwa wahusika walikuwa wakisulubiwa uchi, pia ilikuwa aibu na jambo la kushusha maadili (Mathayo 27:35; Wafilipi 2:8).

Jambo muhimu la Kibiblia kuhusu jinsi alivyokufa ni kwamba, alitimiza unabii. Isaya 53 na Zaburi 22 zinatabiri baadhi ya mambo kuhusu kifo cha Yesu Kristo ambayo yalitimizwa wakati aliposulubiwa. Hata hivyo, kulingana na fungu lililo hapo juu, na nyingine nyingi, ilikuwa ni dhiki ya kiroho pamoja na uchungu wa moyo wa Kristo ambao ulitimila wokovu wetu. Wakati alipofanyika dhambi kwa ajili yetu, alilia, '*Mungu wangu, Mungu wangu, Mbona umeniacha mimi?'* Kulingana na manabii na mitume, wakati kuteseka huku kwa kiroho kulipotokea katika moyo wa Mwokozi, adhabu ya amani yetu ilikuwa inawekelewa juu Yake. Ni wakati huo ambapo alitimiza wokovu wetu. Hii ndio sababu akalia, '*Imekwisha!'* pamoja na, *'Ee ,Baba,*

mikononi mwako naiweka roho yangu.' Wakati mateso au dhiki ilipokwisha, Yeye alitia muhuri msamaha wetu kwa damu Yake (Isaya 53; 2 Wakorintho 5:21; 1 Petro 2:21-25; Yohana 19:30; Luka 23:46). Huu ndio umuhimu wa kweli kwamba 'Wao Wakamsulubisha Yeye.'

Wao Wakamsulubisha Yeye!

Mwishowe, ikiwa tutatilia mkazo neno la kwanza katika maneno haya matatu, basi tutakuwa tukizoa swali kuhusu pingamizi kuu ya Kristo. Ni nani aliyemwua Yesu Kristo? Jibu la kwanza kwa swali hilo wakati mwingi ni kuwa, Warumi ndio waliomwua Yesu Kristo. Lakini hata kama ni askari wa Kirumi ambao walimpigilia misumari na kumdunga kwa mkuki ubavuni mwake Yesu. Tukisoma nakala hiyo vyema, tutakubaliana kwamba ilikuwa ni wa Wayahudi ambao walimsulubisha Yesu Kristo (Mathayo 27:25).

Jibu la Biblia kwa swali hili ni kwamba, ilikuwa ni Mungu ambaye alimfanya mwanawe kuwa dhabihiu kwa dhambi za ulimwengu! Hebu tutazame baadhi ya mifano: Katika sura kuu ya unabii wa Kimasihi, Isaya 53, tunasoma, *'Lakini Bwana alidhirika kumchubua; amemhuzunisha* (Isaya 53:10).' Agano Jipya inasema hivi: '*Yeye (Mungu) asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili ya yetu, hili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye* (2 Wakorintho 5:21).'

Tunahitaji kukumbuka hili wakati tunapotilia maanani kweli kwamba 'Wao walimsulubisha Yeye!'

Ufufuo Wa Yesu (Mathayo 28:1-15)

Ufufuo wa Yesu Kristo unaweza kuthibitishwa na mageuzi yaliyokuwa katika mitume wake pamoja na wanafunzi Wake. Hatuhitaji kumwekea Petro mzigo mzito zaidi, kwa kuwa wakati Yesu alipotiwa nguvuni, tunasoma kwamba 'Wanafunzi wote wakamwacha, wakakimbia (Mathayo 26:56),' Wakati Yesu alipokumbana na pingamizi kuu katika maisha Yake, hakuwa na mfuasi hata mmoja. Uwanachama wa Kanisa wakati huo ulikuwa sufuri!

Ni jambo lipi ambalo lilisababisha 'kule kurudi' kwa Kanisa Lake? Ilikuwa ni ufufuo wa Yesu Kristo.Hii ilikuwa ni kwa sababu alikuwa amewaambia, na pia wao walimsikia akiwaambia kwamba angeuthibitisha Uungu wake baada ya kuuliwa, na kufufuka katika wafu. Tunasoma kwamba: 'Basi alipofufuka katika wafu, wanafunzi wake wakakumbuka ya kuwa alisema hivi, wakaliamini lile andiko na lile Neno alilolinena Yesu (Yohana 2:22).'

Katika mahubiri haya makuu siku ya Pentekoste, Petro aligusia kwamba Agano la Kale lilikuwa limefunza kuhusu ufufuo pamoja na kifo cha Yesu Kristo (Matendo 2:30-32; Zaburi 16). Petro pia alidhihirisha kabisa kwamba miujiza yote na ishara katika siku ya Pentekoste ilikuwa kazi ya Kristo aliyefufuka (Matendo 2:33). Ufufuo wa Yesu Kristo ambao unathibitisha kwamba kifo Chake kilikuwa kwa upatanisho wa dhambi zetu, tunapata tumaini la milele kwa Kanisa siku ya leo (1 Wakorintho 15).

Agizo Kuu (Mathayo 28:18-20)

Jinsi tayari tumeona mara kadha, mpango mwafaka wa Yesu ulikuwa kufikia ulimwengu wote kupitia mitume na wanafunzi wake. Hili linaonekana wazi kwa njia ambayo Injili ya Mathayo inamalizia. Yesu aliwaajibisha na kuwaongoza huku akiwafunza mitume Wake. Na sasa, awapa hotuba ya kuhitimu masomo ya miaka mitatu kwenye Seminari Yake kwa kutoa mwito wakafanye wanafunzi kwa ajili Yake kwa kila kiumbe katika kila taifa ulimenguni.

Agizo Kuu ina amri moja ambayo inaelezewa vyema kwa hatua tatu. Amri hiyo ni: 'Kuwafanya wanafunzi.' Vielelezo ni hivi: Kwenda, kubatiza, na kufunza. 'Huku mnapoenda, kuwabatiza, na kuwafunza mnawafanya wanafunzi' ni tafsiri rahisi na sanifu ya agizo kuu. Kusudi letu wakati tunapoitangaza Injili kwa ulimwengu sio kuwaambia, 'hapa kuna kitu cha bure. Waweza kupokea wokovu kwa kuamini, na kuishi maisha yako jinsi unavyopenda.' Mwito wetu ni kuwafanya kuwa wanafunzi wa Yesu Kristo.

Daktari *Robert S. Glover,* mmishionari mashuhuri na mzalendo mkuu aliandika: ‘Agizo Kuu ni ‘Hati ya uongozi kwa Kanisa.’ Jinsi mashirika mengi yalivyo, Kanisa ni lazima litimize matakwa ya masharti ya hati hiyo ya uongozi au litoweke na lisikuwepo.’

Wasomi wanatuambia kwamba kuna mafunzo mia tano ya Yesu katika Injile nne. Nimeyashiriki tu machache kati ya mafunzo Yake yaliyomo katika utangulizi huu wa vitabu vya Injli na ukaguzi mfupi wa Mathayo. Wakati tunapochambua vyema Agizo Kuu, tutatambua kwamba kufanya wanafunzi kunahusu kuwafunza wale mitume yale yote Yesu aliyowafunza wanafunzi Wake.

Wakati Kanisa lilipofanyika chombo ambacho sio tu cha kuwafanya wanafunzi, bali pia cha kuwafunza, ilikuwa ni Agizo Kuu ambayo ililizaa. Agizo Kuu ilifanya Pentekoste kutokea kwa sababu kusudi lake lilikuwa kuliwezesha Kanisa kutimiza masharti ya hati Yake. Kanisa ndio shirika ulimwenguni liliopo kwa ajili ya wema wa watu ambao sio wanachama wake.

Katika kitabu chetu kifuatacho tutaendelea na ukaguzi wa vitabu vya Injili na naamini kwamba utaendelea kusoma hadithi hii ya historia ya Yesu Kristo. Kwa kumalizia, ningependa kuuliza maswali machache: Je! Wewe umemjia Yesu na kumfahamu kama Mwokozi wako? Je! Una matumaini katika kifo cha Yesu kwa ajili ya malipo ya dhambi yako? Je! Umeuamua kwamba unataka kuwa mwanafunzi, au mfuasi wa Kristo? Utatenda yapi kutokana na yale ambayo umejifunza?

Ombi langu ni kwamba Chuo Cha Biblia kitaendelea kukusaidia kuingia ndani zaidi katika Neno la Mungu na kwamba Neno hilo litaingia ndani yako